# Nipashe

Jumanne Julai 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581011 *

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




DYBALA ATUA RASMI AS ROMA

UKURASA 21

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,016,428,582/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

**Usaili** Sensa ya Watu na Makazi waendelea nchini...

UKURASA 5

# Tahadhari kujikinga ugonjwa wa ajabu

• **Serikali** yabaini unaitwa homa ya Mgunda, SUA walifanyia utafiti... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MPANGO AWAGEUKIA WATAALAMU WA AFYA WANAOHAMISHA DAWA**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali haitawavumilia baadhi ya wataalamu wa afya...

UKURASA WA 7

**MAKALLA AWAONYA WAVAMIZI VIWANJA**



MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewaonya wananchi wanaovamia maeneo ya...

UKURASA WA 19

**RAIS SAMIA AMTUMIA SALAMU ZA RAMBIRAMBI CYRIL RAMAPHOSA**



RAIS wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amemtumia salamu za rambirambi Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa kutokana na kifo...

## Wakili adai hali ya Sabaya yazidi kudhoofu

UKURASA 3





**Kushoto;** aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya akishuka kwenye gari kuelekea mahakamani. **Picha ndogo kulia;** akiwa Mahakama ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kupanda bidhaa kwa athiri mfumuko

UKURASA 3

**MICHEZO** **KOCHA SIMBA ATOA MSIMAMO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner (katikati), Mratibu wa Afya ya Mama na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Dk. Felix Bundala na Mkurugenzi wa Maendeleo FCDO (UKAID), Kemi Williams (kushoto), wakiwa na moja ya maboksi ya dawa za afya ya uzazi zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 4.6 zilizotolewa na shirika hilo kwa wizara hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango aonya wataalamu afya wanaohamisha dawa

**Na Mary Mosha, ROMBO**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali haitawavumilia baadhi ya wataalamu wa afya wamaohamisha dawa kutoka zahanati, vituo vya afya na hospitali za serikali kwenda katika maduka ya dawa.

Alisema miaka ya nyuma baadhi ya maeneo nchini yalikuwa na 'mchwa' katika miradi ya umma, lakini serikali imejizatiti kudhibiti matukio hayo.

Dk. Mpango alisema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi la Hospitali ya Wilaya ya Rombo na kuagiza ianze kazi Oktoba mosi, mwaka huu.

"Ninaamini dawa zitakazoletwa hapa Hospitali ya Wilaya ya Rombo, zitahudumia wananchi kama ilivyokusudiwa, zisipelekwe katika maduka binafsi," alisema.

Aliziomba nchi rafiki, sekta binafsi, mashirika na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi kuisaidia serikali kuboresha sekta hiyo.

Katika hatua nyingine, Dk. Mpango amemwagiza Waziri wa Ujenzi, Profesa Makame Mbarawa, kutangaza zabuni ya ujenzi wa barabara ya Holili/Rotima/Tarakea, yenye urefu wa kilomita 53 ambayo inapita hospitalini hapo.

"Nimeona hospitali hii ipo mbali na makazi ya watu, Profesa Mbarawa popote alipo atangaze zabuni ya barabara hii, kadhalika Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) muitazame barabara hii ipitike mwaka mzima," alisisitiza.

Wakati wa ukamilishaji wa hospitali hiyo ukiendelea, aliitaka Hospitali ya Huruma ambayo ina hadhi ya hospitali ya wilaya, iendelee na hadhi hiyo ili kuhudumia wananchi kikamilifu.

Kadhalika, alimwagiza Mkuu wa Mkoa huo, Stephen Kagaigai kuhakikisha hati ya kiwanja ilipojengwa hospitali hiyo inatunzwa kuepuka wajanja wanaotaka kumega ardhi hiyo.

Kuhusu suala la ukame unaokumba baadhi ya mikoa nchini, Makamu wa Rais, aliomba viongozi wa madhehebu ya dini kuliombea taifa liwe na hali nzuri ya hewa.

"Nitoe Rai kwa viongozi wa dini, kuliombea taifa kupata hali nzuri ya hewa na mvua za kutosha ili tupate mazao na kuondokana na janga la upungufu wa chakula."

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa TAMISEMI, David Silinde alisema kuwa kwa sasa wanaendelea na mpango wa kuboresha huduma za afya ikiwamo uboreshaji wa miundombinu.

Alisema, mpango huo pia unaenda sambamba kuhakikisha vituo vya afya vilivyoko vinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za upasuaji, kukamilisha maboma ya zahanati na kuanza ujenzi wa hospitali za halmashauri ambazo hazina hospitali.

Akitoa taarifa ya mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, alisema mkoa huo unakabiliwa na upungufu wa watumishi katika sekta ya afya kwa asilimia 51.6, uhitaji 8,598 na waliopo ni 4162.

Aidha, alisema ujenzi wa hospitali hiyo utakuwa hatua kubwa katika kuboresha sekta ya afya wilayani Rombo.

Awali, akitoa taarifa ya mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Kanali Hamis Maiga, alisema hospitali hiyo imejengwa katika Kijiji cha Kiwanda, Kata ya Kirongo Samanga, uliogharimu Sh. bilioni 7.9.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo kutanufaisha wananchi zaidi 317,000 ambao walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya.

# Tahadhari kujikinga ugonjwa wa ajabu

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa homa ya Mgunda, ulioibuka na kusababisha vifo vya watu watatu na wengine 10 wakiendelea na matibabu, wilayani Ruangwa mkoani Lindi.

Aidha, ametaja tahadhari wanazopaswa kuchukua wananchi kuwa ni kuepuka kugusa maji au vitu vilivyochafuliwa na mkojo wa wanyama na kunywa maji safi na salama ambayo yamechemshwa au kutibiwa.

Aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake katika wilaya hiyo na kutangaza ugonjwa uliokuwa haujulikani, umejulikana kitaalamu kuwa ni Leptospirosis ambao kwa lugha ya Kiswahili unaitwa ya homa ya Mgunda.

Alisema timu ya wataalamu iligundua kuwa ugonjwa huo kuwa ni miongoni mwa magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na unasababishwa na bakteria aina ya Leptospia interrogans.

"Ugonjwa huu umekuwapo katika maeneo ya kitropiki yenye hali ya joto katika mabara ya Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini, Afrika, Asia na Australia," alisema na kuongeza:

"Wanyama aina ya panya, kindi, mbweha, kulungu, swala na wanyamapori wengine wameripotiwa kupata maambukizi ya vimelea hivi na kuwa chanzo cha maambukizi kwa binadamu," alisema Waziri Ummy.

Kwa mujibu wa mtandao wa Wikipedia, kindi ni wanyama wadogo wa familia ya 'sciuridae' wanaofanana na nguchiro, vicheche ambao hula mbegu, makokwa, wadudu, ndege, mayai na matunda.

**UNAVYOAMBUKIZWA**

Waziri Ummy, alisema ugonjwa huo huambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kupitia uchafuzi wa mazingira, ikiwamo vyanzo vya maji kutoka katika mkojo wa wanyama wenye maambukizi.

Alifafanua kuwa mtu anaweza kuambukizwa kwa kugusa majimaji yenye vimelea vya ugonjwa huo, ikiwamo kugusa udongo, kula chakula kilichochafuliwa na au kunywa maji yaliyochafuliwa na mkojo wa wanyama wenye vimelea vya bakteria wa ugonjwa huo.

Hata hivyo, alisema maambukizi ya ugonjwa huo kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine hutokea kwa nadra.

Aliwataka wagonjwa wenye dalili za homa, kuvuja damu, kichwa kuuma na mwili kuchoka kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, ili wapate matibabu sahihi.

"Wizara inaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na ugonjwa huu na kuendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa ugonjwa huu. Hivyo serikali inawaasa wananchi kutokuwa na hofu kwani ugonjwa huu unaendelea kudhibitiwa," alisema Waziri Ummy.

**SUA WALITAHADHARISHA**

Septemba mwaka jana, Nipashe iliripoti wasilisho la ripoti ya wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) uliofanyika kwa miaka 25 chini ya ufadhili wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) iliyoonyesha kuwapo ongezeko la ugonjwa huo kwa binadamu kwa idadi kubwa katika mikoa mingi ikiwamo Morogoro, Kilimanjaro na Katavi.

Aidha, utafiti huo uliofanyika kuanzia mwaka 1996 pia ulionyesha kuwa kulikuwa na kiwango kikubwa cha Leptospirosis mkoani Morogoro (asilimia 10.8-13) mwaka 2015 na Kilimanjaro (asilimia 9-20) mwaka 2013.

Kutokana na ripoti hiyo, wataalamu hao waliishauri serikali na wadau wa afya kuchukua hatua za haraka kukabiliana na ugonjwa wa homa ya Lesptospirosis, ambao wamebaini haufahamiki kwa wengi, lakini unasambaa na kuathiri binadamu na wanyama nchini.

Dk. Abdul Katakweba wa SUA, aliyekuwa sehemu ya utafiti huo, alisema ugonjwa huo unaosababishwa na bakteria anayeitwa Leptospira na unaenezwa kupitia kwa wanyama na kuaambukizwa kupitia udongo wenye unyevunyevu (tope) na maji, ambamo bakteria huyo anaweza kukaa kwa muda mrefu.

Wataalamu hao walitahadharisha kuwa kulingana na ripoti hiyo, kuna hatari kubwa ya maambukizi ya kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu nchini, ikizingatiwa asilimia 70 ya raia wanajihusisha na shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi.

"Bakteria husambazwa kwa binadamu na panya na mamalia wengine wadogo kwa kugusa mkojo wao wenye vimelea, nyama na vingine vyenye majimaji," ilisomeka sehemu ya ripoti hiyo ya utafiti.

Watafiti hao walisema licha ya ukweli kwamba ugonjwa huo unaweza kutibiwa kwa dawa, ukosefu wa miongozo na usimamizi wake nchini, unaweka watu wengi katika hatari ya kuugua na hata vifo.

Wataalamu hao wa SUA walisema dalili za Leptospirosis ni sawa na za magonjwa mengi ya homa, ni muhimu kuwa na miongozo inayofaa kwa watoa huduma za afya juu ya usimamizi wake ili kuzuia vifo na kuokoa rasilimali zinazotumika isivyofaa kutibu maradhi mengine ilhali kumbe mgonjwa ana Leptospirosis.

"Ni wakati mwafaka watoa huduma za afya wawe na uelewa wa uwapo wa Leptospirosis na vituo vya afya viwe na vifaa vinavyohitajika kutambua na kutibu ugonjwa huu," wataalamu hao walipendekeza katika ripoti yao hiyo ya utafiti.

Walisema kuwa utafiti huo ulibaini kuwa magonjwa mengi ya homa yanahusishwa na malaria hali inayowafanya watu wengi kuwa kwenye hatari ya kupoteza maisha kutokana na kupewa matibabu ya ugonjwa huo tofauti na wanachougua.

Wataalamu hao wa SUA wanashauri miongozo ya udhibiti na matibabu ya magonjwa ya homa, izingatie uwezakano wa kuwapo kwa magonjwa mengine yanayofanana na hayo ya homa, ikiwamo Leptospirosis.

HABARI KITAIFA

# Wakili adai afya ya Sabaya yazidi kudhoofu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake wanne, umeeleza kusikitishwa na taarifa za kutokamilika kwa upelelezi na kukosekana kwa kibali cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi kusikiliza kesi hiyo.

Aidha, umedai hofu yao ya kutosikilizwa kwa kesi hiyo iwapo mshtakiwa Ole Sabaya, ataendelea kudhoofika zaidi kiafya kutokana na kutoa taarifa awali ya mshtakiwa huyo kuwa mgonjwa sana.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya wilaya, Elibariki Philli, anayesikiliza kesi hiyo, Wakili wa Utetezi, Helen Mahuna, alidai kuwa ni siku 48 sasa, upande wa Jamhuri unatoa sababu ya aina moja jambo linalochelewesha kuanza kesi hiyo.

Katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi, Wakili Mahuna aliutaka upande wa Jamhuri kusimamia kauli yake ya awali wakati kesi hiyo ikifunguliwa.

"Mheshimiwa hakimu, bado tunaiomba mahakama yako tukufu iuelekeze upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi pamoja na kibali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), ili kusikiliza kesi hii, mshtakiwa ni mgonjwa akizidiwa hapa kesi haitasikilizwa tena," alidai.

Wakili Mahuna aliyeambatana na Wakili Fauzia Akonay, aliuomba upande wa Jamhuri kukamilisha taratibu hizo ili washtakiwa wote watano kwa pamoja waweze kupata haki zao kwa madai kuwa kwa sasa wanateseka mahabusu.

Wakili Mahuna alidai, awali wakati wa kufunguliwa kwa kesi hiyo, upande wa Jamhuri uliieleza mahakama kwamba upelelezi umekamilika, lakini sasa umebadili kauli na kudai bado haujakamilika.

Katika maombi yake ya msingi, Wakili wa Jamhuri, Sabitina Mcharo, aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine kutokana na kutokamilika kwa upelelezi na pia kutopata kibali kutoka kwa DPP cha kuipa mahakama hiyo hadhi ya kusikilikiza kesi hiyo.

Kutokana na kauli hiyo, hakimu Philli aliuhoji upande wa Jamhuri kujua kama upelelezi umekamilika, jibu lilikuwa upelelezi haujakamilika na upatikanaji wa kibali kutoka kwa DPP.

Hakimu Philli pia alihoji tukio linadaiwa kutokea mwezi Februari, 2021, suala linalokwamisha kesi ni upelelezi au kibali kutoka kwa DPP, kauli iliyojibiwa na Jamhuri kwamba vyote kwa pamoja havijakamilika.

Baada ya majibizano hayo, Hakimu Philli aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 29, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa rumande.





Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Bimkuwa Nassor (kulia), mwakilishi wa kikundi cha wakulima wa Mwani cha Subira Nzuri baada ya kukabidhi vifaa vya uvuvi pamoja na boti za kupakilia mwani akiwa katika ziara ya Wilaya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi. **PICHA: IKULU**

# Kupanda bidhaa kulivyoathiri mfumuko wa bei

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MFUMUKO wa bei kwa mwezi Juni, mwaka huu, umeongezeka hadi asilimia 4.4 kutoka asilimia 4.0 ya mwezi Mei, mwaka huu.

Miongoni mwa sababu ni kupanda kwa bei ya baadhi ya bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula.

Kwa mujibu wa taarifa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kuhusu mfumuko wa bei, bidhaa zilizooongeza mfumuko huo kwa mwezi Juni, mwaka huu na asilimia zake kwenye mabano ni nafaka za ngano (0.9), mchele (1.3), nafaka za mahindi (5.4), unga wa ngano (1.2), unga wa mahindi (6.4), mboga (1.1), viazi mviringo (10.2).

Pia muhogo (6.3), maharagwe (0.9), unga wa muhogo (4.6) na vinywaji baridi (soda 0.7).

Kwa upande mwingine, ofisi hiyo ilisema baadhi ya vitu visivyo vya chakula ambavyo vilichangia kuongezeka kwa fahirisi ya bei ni saruji (0.5), bati (8.1), gesi (6.3), mafuta ya taa (5.7), sabuni ya kufulia (2.2), sabuni ya unga (7.2), nauli ya basi (4.2), usafiri wa teksi (3.6) na nauli ya pikipiki (bodaboda 5.6).

Hata hivyo, taarifa hiyo ilionesha kuwa mfumuko wa bei wa chakula na vinywaji visivyo na pombe kwa Juni, 2022 umeongezeka hadi asilimia 5.9 kutoka 5.5 Mei, 2022.


SOS CHILDREN'S VILLAGES

**Tender No. SOSCV/AR/2022/DITCH/01**

**For**

**The purchase of Brand New Program Vehicles – Toyota Land cruiser Hard Top five doors with bull bar winch for SOS Children's Village Arusha**

## Invitation for Tenders

**Date: 18/07/2022**

1. The SOS Children's Village has set aside funds to procure two program Vehicles Toyota Land Cruiser Hardtop five doors with bull bar winch

2. The SOS Children's Village now invites sealed tenders from various registered firms for the supply of the vehicles

3. You may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at SOS Children's Village Arusha located at Ngaramtoni within Arusha District Council at Arusha P.O. Box 13196 Arusha from 0800 hrs to 1700 hrs on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

4. Tendering will be conducted through SOS Procurement Policy.

5. A complete set of Tendering Document(s) in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers upon submission of a written application to the address given under paragraph 3 above and upon payment of a non-refundable fee of TZS: 50,000= Or it's equivalent.

All payments to be done directly to ABSA Bank, Ohio Branch, SOS Children's Villages Tanzania Trust, A/C 001-4009337

Deposit slip to be submitted with tender documents to SOS Children's Village Arusha located at Ngaramtoni – Arusha District Council P.O. Box 13196 Arusha

6. All Tenders must be accompanied by a tender securing declaration in the form provided in the tender forms

7. All tenders, one original plus three copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes clearly marked **"TENDER NO. SOSCV/AR/2022/DITCH/01 FOR THE PURCHASE OF BRAND NEW PROGRAM VEHICLES – TOYOTA LAND CRUISER HARD TOP FIVE DOORS WITH A BULL BAR WINCH FOR SOS CHILDREN'S VILLAGE ARUSHA** Should be addressed to SOS CHILDREN'S VILLAGE, P.O. BOX 13196 Arusha Tanzania to reach at SOS CHILDRENS VILLAGE within Fourteen (14) calendar days. Tenders will be opened thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at SOS CHILDREN VILLAGE AT NGARAMTONI WITHIN ARUSHA DISTRICT AT ARUSHA

8. Late Tenders, Portion of Tenders, Electronic Tenders, Tenders not received, Tenders not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**PROCUREMENT COMMITTEE,**
**SOS CHILDREN'S VILLAGES, P.O. BOX 13196**
**ARUSHA, TANZANIA**

216948201



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima (katikati), akisisitiza jambo wakati akikagua maeneo yaliyovamiwa na wananchi katika shamba la Amboni jijini Tanga, (kulia) ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa, Mstahiki Meya wa Jiji, Abdulrahman Shiloow (kushoto), na mwenye shati la njano ni Katibu wa CCM Mkoa, Suleiman Mzee. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Taasisi kilimo hai Afrika kukutana Rwanda

**Na Faustine Feliciane**

TAASISI zinazojishughulisha na kuendeleza kilimo hai nchini zimeaswa kujitokeza kushiriki kwenye mkutano mkubwa wa kilimo hai Afrika utakaofanyika jijini Kigali, nchini Rwanda kuanzia Novemba 9 - 12, mwaka huu.

Mkutano huo unaandaliwa na mtandao wa kuendeleza Kilimo hai Afrika (Afronet) na nchi mbalimbali za Afrika zitashiriki kupitia taasisi za kitaifa za kilimo hai na binafsi.

Mkutano huo unaandaliwa na Afronet chini ya mradi wake wa kusimamia na kuendeleza kilimo hai wa IIABA unaoendeshwa kwenye nchi mbalimbali Afrika, Tanzania ikiwamo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mratibu Mwandamizi wa mradi huo wa IIABA kutoka Afronet, Mgeta Daudi, alisema mkutano huo utakutanisha wadau mbalimbali wa kilimo hai kutoka nchi za Afrika ambayo Afronet inatekeleza miradi yake.

"Kwa hapa nyumbani Tanzania kuna taasisi nyingi za kilimo hai chini zote hizi zinaweza kushiriki kwenye mkutano huu, ni vizuri kwa taasisi nyingi za hapa Tanzania kushiriki mkutano huu kupata elimu na taarifa mbalimbali zitakazosaidia taifa kupambana na kilimo cha kemikali ambapo baadhi ya kemikali hizo zinaua ardhi yetu, lakini zinafanya kuzalisha chakula chenye sumu," alisema Daudi.

Alisema kuwa taasisi za serikali zinazojihusisha na masuala ya kilimo zitashiriki mkutano huu.

Akizungumzia mradi wa IIABA, Daudi alisema, ulizinduliwa Desemba 14, 2019 na kuanza kazi rasmi Februari 2020 na utafikia mwisho mwakani.

"Lengo la mradi huu ni kuchagiza ukuaji wa sekta ya kilimo hai na kuinua ubunifu kwenye sekta hiyo, lakini kuzijengea uwezo taasisi za kilimo hai kushiriki shughuli hizo kimataifa," alisema Daudi.

Kwa upande wake, ofisa habari wa Afronet Tanzania ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Constantine Akitanda, alisema taasisi hiyo imebaini kemikali za kilimo zinatumiwa isivyo sahihi na kusababisha madhara mbalimbali kwenye ardhi na afya ya mtumiaji wa mazao yanayozalishwa kwa kemikali.

"Tunataka watu wajue matumizi sahihi ya kemikali, tunaamini nyingi hazitumiki sahihi, mradi huu unatoa elimu na kuhamasisha kilimo hai, tunaamini ndiyo kilimo sahihi kwa mustakabali wa ustawi wa maisha yetu," alisema Akitanda.

Kama taasisi wanafurahi kuona kwa sasa Tanzania ipo kwenye mkakati wa kuanzisha sera ya taifa ya kilimo hai na tayari kamati iliyoundwa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo ipo kazini.

# Benki ya Exim yainunua FNB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania, imetangaza rasmi kuinunua iliyokuwa Benki ya FNB Tanzania, ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wa kujitanua zaidi ndani na nje ya mipaka ya nchi.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya kuwakaribisha wateja wa iliyokuwa Benki ya FNB Tanzania, iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu, alisema hatua hiyo imekuja kutokana na kukamilika kwa mafanikio makubwa kwa mchakato wa umiliki wa benki hiyo chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Alisema ununuzi wa benki hiyo umekuja miaka mitatu tangu iliponunua Benki ya UBL Tanzania.

"Ununuzi wetu wa Benki ya FNB Tanzania unatuwezesha kuongeza idadi ya wateja watakaofikiwa na huduma za Benki ya Exim ndani na nje ya nchi. Tukiwa tunaelekea kuadhimisha miaka 25 ya kuanzishwa kwa benki hii, tunajivunia ukuaji huu unaotupa hadhi ya kuwa benki kimbilio sio tu Tanzania bali pia nje ya nchi ambapo pia tunaendelea kujitanua," alisema.

Pia ina matawi katika nchi za Uganda, Djibouti, Comoros na Ethiopia.

Mpaka sasa, Benki ya Exim iko miongoni mwa benki tano bora nchini yenye mali za tabriban Sh. trilioni 2.4 kwa ujumla katika nchi zote nne.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza, imeendelea kufanya vizuri sokoni kwa kuzalisha faida ya kabla ya kodi ya Sh. bilioni 18, ikilinganishwa na Shilingi bilioni sita iliyopatikana katika nusu ya kwanza, mwaka jana.

Matundu alisema ukuaji wao wa jumla ya mali hadi Sh. trilioni 1.5 kutoka Sh. trilioni 1.3 i mwaka uliopita na dhamana za wateja kutoka Sh. bilioni 780, Juni mwaka jana hadi Sh. bilioni 943 Juni mwaka huu.

## HABARI KITAIFA

# Usaili makarani wa sensa

**Na Jenifer Gilla**

KAMISAA wa Sensa Tanzania Bara, Anne Makinda, amesema kuwa usaili wa waombaji 600,000 wa ukarani kwenye Sensa ya Watu na Makazi, unaendelea na wanatarajiwa kupatiwa mafunzo wiki ijayo.

Akizungumza na Nipashe, Makinda ambaye ni Spika mstaafu, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na mafunzo yanayoendelea sasa ni kwa wakufunzi wa makarani watakaofanya kazi hiyo Agosti 23, mwaka huu.

Alisema mafunzo ya wakufunzi hao yanafanyika katika ngazi ya mikoa na watakwenda kuwafundisha makarani hao ngazi ya wilaya.

"Tulianza na wakufunzi wa kitaifa, mafunzo yao yalifungwa na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Hemed Suleiman Abdalla). Baada ya hapo yakaanza mafundisho ya wakufunzi wa mikoa ambayo ndiyo inaendelea sasa mikoa yote, hawa wanamaliza Julai 26, Julai 29, mwaka huu, wanaanza kuwafundisha wale makarani ambao watateuliwa," alibainisha Makinda.

Alisema dirisha la maombi lilifungwa miezi miwili iliyopita, sasa kinachofuata ni usaili kwa waombaji wa nafasi hizo na wale watakaofaulu wataanza mafunzo Julai 29 hadi Agosti 18, mwaka huu.

"Sasa kinachoendelea ni usaili wa makarani, kwa sababu walijaza online (kwenye mtandao), wanatakiwa waonekane 'physically' (uso kwa uso) na waweze kujibu maswali watakayoulizwa yaliyoandaliwa na vyuo vya takwimu vilivyoko nchini," alibainisha.

Mei 20, mwaka huu, akitoa taarifa ya waombaji wa kazi hizo, Makinda alisema kuwa jumla ya watu 674,884 waliomba kufanya kazi hiyo ya muda huku wanaohitajika wakiwa ni 205,000.

Aidha, alisema elimu na uhamasishaji bado inaendelea kutolewa mpaka itakapofika siku ya sensa ambayo ni Agosti 23, mwaka huu, ili kuendelea kuijengea jamii uelewa juu ya umuhimu wa siku hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Mtakwimu ya Taifa (NBS), kwenye tovuti yake, ilieleza kuwa utekelezaji wa sensa ya watu na makazi utafanyika katika awamu tatu ambazo ni kabla ya kuhesabu watu, wakati wa kuhesabu na baada ya kuhesabu.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa kipindi cha kabla ya kuhesabu watu kinajumuisha mambo mbalimbali, ikiwamo uandaaji wa kitabu cha mkakati wa usimamizi na utekelezaji wa sensa na nyaraka nyingine.

Pia, utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu na uzalishaji wa ramani na uandaaji wa madodoso na miongozo mbalimbali na uhamasishaji.



Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi Matari Masige, wakati alipokagua maendeleo ya mradi wa kufungua (open up) barabara ya Luteba hadi Ipelele ya kilomita 9 inayounganisha Wilaya za Makete (Njombe) na Rungwe (Mbeya), mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania waonyeshwa mlango soko Afrika

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wametakiwa kujiandaa kuingia kwenye soko la nchi za Afrika kwa kutengeneza bidhaa zenye ubora na bei nafuu.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Christopher Mramba, kwenye hafla ya utoaji wa tuzo za kitaifa za ubora kwa washindi wa mwaka 2021/2022.

Alisema hilo litafanikiwa ikiwa bidhaa na huduma kutoka Tanzania zitakuwa zenye ubora wa hali ya juu.

Mramba alisema kutokana na makubaliano baina ya wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo kwa nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), tuzo za ubora zilianzishwa ili kutambua na kukuza sekta ya biashara kupitia ubora wa bidhaa na huduma katika ukanda huo.

"Kwa sababu hiyo serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara iliona umuhimu wa kuanzisha tuzo za ubora za kitaifa na kutoa jukumu la kuziratibu kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na TPSF," alisema Mramba.

Alifafanua kwamba utoaji wa tuzo hizo ni ishara ya kukamilika kwa mchakato wa ubora kwa mwaka 2021/2022 na kukamilika ni mwanzo wa msimu mpya wa kitaifa wa ubora kwa mwaka 2022/2023.

Kaimu Mkurugenzi wa TBS, David Ndibalema, alitoa wito kwa wazalishaji na watoa huduma kutambua njia bora ya kulinda soko la bidhaa na huduma za ndani na nje ya mipaka ni kuzalisha bidhaa na kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu na kwa gharama nafuu.

Ndibalema alisema wazalishaji na watoa huduma wanahitajika kujengewa au kujijengea utamaduni wa ubora na ushindani nchini.

"Vilevile, wanahitaji kufahamu uhusiano kati ya ubora na ushindani hii ndiyo njia pekee kwa nchi yetu kusonga mbele kibiashara, hasa katika mapinduzi ya nne ya viwanda," alisema Ndibalema.

Moja ya hatua zilizochukuliwa na serikali ili kujenga utamaduni wa kuthamini ubora kwenye jamii ni kuanzisha tuzo za kitaifa za ubora.

"Tuzo hizi zinafanyika ikiwa ni msimu wa pili na lengo la kuwatambua na kuwapongeza watu binafsi pamoja na taasisi zinazofanya vizuri kwenye masuala ya ubora wakati wa utekelezaji wa shughuli zao za uzalishaji bidhaa au utoaji huduma," alisema.

"Lengo lingine kufanyika kwa tuzo hizi ni kuhamasisha ubunifu na uboreshaji wa bidhaa na huduma zinazotolewa hapa nchini kupitia taratibu zilizowekwa chini ya miundombinu ya ubora," alisema Ndibalema.

Akizungumzia tuzo hizo, Ndibalema alisema kwa mwaka 2021/2022 ziliandaliwa kwenye vipengele vitano, cha kwanza ni tuzo kwa kampuni bora ya mwaka, ya pili ni kwa bidhaa bora ya mwaka, ya tatu ni kwa huduma bora ya mwaka, ya nne ni muuzaji bora wa bidhaa nje ya nchi na tano ni kwa mtu mmoja aliyefanya vizuri kwenye masuala ya ubora.

Kwa kipengele cha kwanza hadi cha nne, alisema ziliandaliwa tuzo kwenye makundi mawili kwa kila kipengele, ikiwamo ya kampuni kubwa na pia kwa kampuni ndogo au wajasiriamali wadogo. Kipengele cha tano kinahusisha tuzo moja kwa mtu mmoja pekee.

Mashindano ya tuzo kwa msimu wa mwaka 2021/2022 yamekuwa ni yenye mwamko mkubwa kutoka kwa washiriki ambapo vipengele vyote vilipata washiriki na washindi ikilinganishwa na msimu uliopita wa mwaka 2020/2021, baadhi ya vipengele kukosa washiriki.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuungane na maaskofu tunusuru mazingira

**WANACHAMA** wa Mabaraza ya Maaskofu Katoliki wa Afrika Mashariki na Kati (AMECEA), wamemaliza mkutano wao Dar es Salaam, unaotuachia somo la kuhifadhi mazingira ili tusiangamie.

AMECEA iliyokutana kujadili ajenda kuu ya ulinzi na utunzaji wa mazingira, tunawapongeza wanachama wake kujitokeza na kueleza waziwazi kuwa kama taifa na dunia hatutalinda na kuhifadhi mazingira kuna hatari ya kuangamia nasi tukiwa waathirika.

Wanachama wa mabaraza hayo kutoka Ethiopia, Eritrea, Kenya, Malawi, Tanzania, Uganda, Sudani na Sudani ya Kusini, Zambia na waalikwa kutoka Djibouti na Somalia wametafakari mzigo mkubwa unaozielemea nchi zao kutokana na uharibifu wa mazingira na kukemea tabia ya mwanadamu ya kuharibu maumbile.

Baadhi ya changamoto za uharibifu wa mazingira zinazotajwa na maaskofu ni nyingi kama ukame na njaa za mara kwa mara, upepo na vimbunga, mvua zisizotabirika, mafuriko, wadudu kama nzige ambao hata mwaka huu walionekana kwenye ukanda wa AMECEA.

Wakati mkutano huo, umemalizika Dar es Salaam juzi, upatikanaji wa mahindi katika mikoa mingi mwaka huu ni changamoto, mazao mengine kama mpunga pia yamekwamishwa na ukame.

Tukiangalia huduma muhimu za kijamii kama maji zinaendelea kuwa tatizo kutokana na vyanzo vingi kuharibika. Siyo siri, mito mingi inakauka, mabwawa na hata maziwa kama Rukwa nayo yamepungua kina, aina kadhaa za samaki zimetoweka.

Aidha, maziwa mengine makubwa kama Victoria na Tanganyika kina kinaongezeka kutokana na sababu kadhaa lakini mojawapo ni kujaa tope (silt) na taka.

Kadhalika, misitu ya asili iliyokuwa vyanzo vya maji na mito mikubwa vimekuwa makao ya taka za plastiki na hata za kilimo na za sumu mathalani, Ziwa Victoria.

Hii ni rasilimali inayotumiwa na nchi wanachama wa AMECEA, kuanzia Tanzania, Uganda na Kenya lakini ni chanzo cha Mto Nile unapita Ethiopia, Sudan, Sudan Kusini, hadi Bahari ya Mediteranian.

Maji yake ni muhimu kwa maendeleo ya nchi nyingi za Afrika, kadhalika Ziwa Victoria nalo lina umuhimu wa kipekee kwa kuwa ni mama kwa Mto Nile, hivyo linahitaji kulindwa na kutunzwa vingine kama AMECEA wanavyosema kuna kitisho cha dunia kutoweka kutokana na uharibifu wa mazingira unaotishia hatima ya watu na viumbe kama wanyama, mimea, wadudu na hewa angani.

Tunaona kuwa wanachosema maaskofu hawa ni ukweli, wanaeleza kuwa kunahitajika mikakati mipya ya kichungaji, kitaifa, kikanda na kimataifa ili kulinda ikolojia ambao ni uhusiano wa binadamu na mazingira na kuzuia mabadiliko zaidi ya tabia nchi ambayo yasipodhibitiwa yataathiri kila mtu.

Mikakati na matendo ili tuweze kusafiri kwa pamoja katika nia ya kubadilika katika Kanda ya Afrika Mashariki na kote Afrika inahitajika, mojawapo ni kuzuia mizozo na vita vinavyoathiri mazingira na kuongeza umaskini kutokana na kukosekana chakula, malisho ya wanyama, ardhi ya kilimo, maji na hata kuibuka maradhi.

Tunaungana na serikali na maaskofu kusisitiza kulinda na kutunza mazingira kwa kuwahamasisha watu kubadilika na kufahamu kuwa mabadiliko ya tabianchi siyo hadithi wala ndoto ni ukweli unaoonekana kwenye ukame, mafuriko na vimbunga vinavyowatesa hata sasa.

Tunaisihi jamii kuacha kukata misitu kwani kasi ya misitu ya asili kutoweka inatisha. Ili kukabiliana uhaba wa nishati ya kupikia serikali isaidie kwa kutoa ruzuku ya gesi, umeme na vifaa vya kupikia ili kupunguza na mwisho kuacha matumizi ya kuni na kuchoma mkaa.

Aidha, kuanzia sasa kuwe na kampeni kabambe za kupanda miti ya asili inayolinda maji, ardhi, pia kuhifadhi, misitu, maji, viumbe na kufundisha elimu ya mazingira kwa kina ili kuiokoa Tanzania na mabadiliko ya tabia nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kambi za taaluma ziimarishwe kuinua elimu



Na Sabato Kasika

**UWAPO** wa kambi za kitaaluma umechangia wanafunzi katika maendeleo ya elimu kwa kuwawezesha kufanya vizuri kwenye mitihani yao na kuwapa uhakika wa kusonga mbele kielimu.

Hiyo, inatokana na ukweli kwamba, wanafunzi ambao wamewahi kukaa makambini kwenye baadhi ya mikoa, walifanya vizuri na hivyo kuwawezesha kuendelea na masomo.

Wanafunzi hao ni wale wa shule za msingi na sekondari, ambao wamewahi kuwekwa katika kambi hizo lengo likiwa ni kuhakikisha ufaulu unaongezeka, ambapo kambi hizo zilisaidia kuleta matokeo chanya.

Hata hivyo, kwa sasa kampeni za kuhamasisha kambi hizo ni kama zimefifia, kwani hamasa zilizokuwapo katika mikoa mbalimbali miaka michache iliyopita hazisikiki tena, hali inaonyesha huenda wahamasishaji wamerudi nyuma.

Mkoa wa Simiyu chini ya Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, uliasisi kambi hizo kwa kushirikiana na wadau wengine wa elimu wa mkoa huo na kuibua kambi hizo za kitaaluma, hatua ambayo ilielezwa kuongeza ufaulu.

Kambi hizo ziliandaliwa kwa ushirikiano kati ya shule na wadau mbalimbali wa elimu wakiwamo wazazi na walezi, ambao walikuwa wakichangia vyakula na fedha ili kuhakikisha zinaimarika.

Mkoa huo uliwahi kushika nafasi ya 10 kitaifa katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha sita mwaka 2018, kutoka nafasi ya 26 mwaka 2017 ambapo mkoa uliendelea kuimarisha kambi hizo.

Ni wazi kwamba, wanafunzi kuwekwa kambini wanapata muda mwingi wa kujifunza na kujisomea, hali ambayo kwa namna moja au nyingine imasaidia kuongeza ari ya kupenda elimu na kuongeza ufaulu.

Ipo mikoa mingine ilioiga mfumo huo wa kambi za kitaaluma, lakini ninadhani kwamba zimeanza kufifia, kwani hazisikiki kama zamani, hali inayoonyesha kuwa huenda zimeachwa.

Ninaamini kuwa katika mazingira ya nyumbani kwa baadhi ya wanafunzi, hayawapi nafasi ya kujisomea wanaporudi nyumbani au siku za mwisho wa wiki, hivyo kambi hizo zilikuwa njia mojawapo ya kuwawezesha kusoma.

**Ni wazi kwamba, wanafunzi kuwekwa kambini wanapata muda mwingi wa kujifunza na kujisomea**

Wakati mwingine, kwa wanafunzi wa shule za vijijini, wanaweza kujikuta mwisho wa wiki wanapewa jukumu la kwenda kuchunga ng'ombe, kulima na shughuli nyingine za nyumbani, ambazo nazo ni muhimu, lakini ni vyema wakawa na muda wa kujisomea.

Njia mojawapo ya kuwafanya wawe na muda wa kujisomea, ni hiyo ya kambi za kitaaluma, lakini nazo ni kama zimeanza kufifia, hivyo si vibaya waanzilishi wakaangalia ni wapi walikosea ili kuziwezesha kuwa na nguvu.

Ninaamini kwamba, mzazi au mlezi anayejua umuhimu wa elimu atakuwa tayari kuchangia kwa ajili ya kusaidia kuinua kiwango cha elimu cha mtoto wake ili aweze kusonga mbele katika masomo ya juu.

Elimu ni ufunguo maisha, elimu ni mali, dhana hizi na nyingine nyingi zinaonyesha jinsi elimu ilivyo ya muhimu kwa mwanadamu na ndiyo maana wale wanaowakatiza wanafunzi masomo huchulikuwa hatua za kisheria.

Kwa maana hiyo, ninadhani ipo haja ya kufufua kambi hizo, hasa kwa kuzingatia kwamba kule zilizoanzia zilisaidia kuwafanya wanafunzi kupata matokeo chanya katika mitihani ya taifa.

Uwapo wa kambi hizo mkoani Simiyu, ulichagizwa na zawadi kwa wanafunzi waliokuwa wakipata matokeo mazuri, hali ambayo iliwafanya wawe na hamasa katika masomo shuleni.

Hata baadhi ya wanafunzi walikuwa wakikiri kwamba, kambi hizo zilikuwa msaada mkubwa kwa kwao hasa wale waliokuwa wakitoka katika mazingira magumu ambayo yaliyowafanya wasiwe huru kujisomea.

Aidha, kambi hizo pia zilikuwa msaada kwa wanafunzi wa kike kuepukana na vishawishi hasa wale waliokuwa wakitembea umbali mrefu kwenda shule na kurudi nyumbani ambapo kukaa sehemu moja kulikuwa ni nafuu kwao.

Kambi za kitaaluma zimeishia wapi? Kwa nini hazisikiki kama zamani? Kama zimekumbwa na changamoto, kwa nini changamoto hizo zisitafutiwe ufumbuzi ili ziendelee kusaidia wanafunzi?

Mbinu za ufaulu zipo nyingi, mojawapo ikiwa ni hiyo ya wanafunzi kuwekwa katika kambi ambazo kimsingi zilisaidia wanafunzi kufanya vizuri. Nadhani matarajio yangekuwa ni kuenea kwa kambi hizo nchi nzima.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Yuhoma Education Limited, Yusuph Yahaya (kushoto), akitoa maelezo namna chuo hicho kinavyotoa mkopo wa kusoma nje ya nchi, kwenye maonyesho ya 17 ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia, yanayofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Watanzania waambiwa kuandika wosia sio uchuro

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema mwamko wa Watanzania kuandika wosia ni mdogo na kuuagiza Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), kufanya tathmini ya kina kubainisha sababu zinazochangia wananchi kutokuandika.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, wakati akifungua kikao cha utoaji huduma bora na endelevu kilichofanyika jana Dar es Salaam.

Alisema tatizo hilo la kutoandika wosia linaendelea kuchangia migogoro mingi katika familia huku waathirika wakubwa wakiwa ni wanawake na watoto.

"RITA inatoa huduma ya kuandika na kutunza wosia, lakini bado mwamko wa wananchi kuandika wosia huo nchini sio wa kuridhisha na hivyo kuendelea kusababisha migogoro katika jamii ambayo kwa kiasi kikubwa inawaathiri kinamama na watoto," alisema Makondo.

"Tayari wizara tumekwishatoa maelekezo kwa RITA kufanya tathmini ya kina kubainisha sababu zinazochangia wananchi kutoandika wosia na tayari dodoso limeshaandaliwa kwa ajili ya kuanza kukusanya taarifa."

Alizungumzia kuwapo imani potofu kwenye jamii kuwa kuandika wosia ni uchuro na kuziomba taasisi za dini kusaidiana na serikali kuelimisha wananchi kuondokana na imani hizo.

"Bado kuna baadhi ya Watanzania ambao wanaamini kwamba kuandika wosia ni uchuro, hii sio kweli. Unapoandika wosia inasidia kuweka vitu sawa hata kama ni mali na kufanya hivyo kunachangia kuondoa migogoro kwenye familia, kwa hiyo ninashauri watu kuondokana na imani hizo, waandike wosia, na tumewaagiza RITA wafanye tathmini ya kina na watupe mrejesho wa yale yanayosababisha watu wasiandike," alisema Makondo.

Kwa upande wake, Kabidhi Wasii Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Angela Anatory, alisema bado kunahitajika ushiriki wa wadau mbalimbali katika kufanikisha malengo yaliyokusudiwa utoaji wa huduma kwa wakala huyo.

"Tunafanya vikao kama hivi na wadau, kuwashirikisha mengi yaliyofanyika, lakini pia kupata mchango wao namna ya kuendelea kuboresha zaidi," alisema Anatory.

Mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Maud Fortuijn, alisema wameshuhudia kazi kubwa iliyofanywa na RITA hususani kupitia programu ya usajili wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano na kuahidi kuendelea kushirikiana nao katika kazi hiyo.

# Bashe aunda kamati kutatua changamoto sekta ya sukari

**Na Renatha Msungu**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ameunda kamati itakayopitia mfumo wa uzalishaji pamoja na mchakato wa ugavi utakaotumika katika sekta ya sukari wilayani Kilombero ili kusaidia kupatikana mwarobaini wa tatizo lililoko.

Waziri Bashe ameteua kamati hiyo wakati wa mkutano na wakulima wa miwa wa mashamba ya Kilombero uliofanyika wilayani humo mkoani Morogoro.

Alisema kamati hiyo itaongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerard Mweli, pamoja na wajumbe wengine ambao watashirikiana kwa ajili ya kuhakikisha changamoto zilizoko ndani ya sekta hiyo zinatatuliwa.

"Naomba hii kamati mkafanye kazi vizuri ili kutatua changamoto zilizoko ndani ya sekta ya sukari," alisema Bashe.

Alitoa agizo kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika pamoja na Kampuni ya Sukari ya Kilombero kufanya usanifu wa kina ili serikali itengeneze miuondombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wa miwa. Alifafanua kuwa serikali itaanzisha kitalu cha kuzalisha mbegu za miwa wilayani Kilombero ili kuongeza uzalishaji katika sekta ya sukari.

"Serikali inatarajia kuanzisha kitalu cha kuzalisha mbegu za miwa lengo ni kuhakikisha mbegu bora zinapatikana," alisema Bashe.

Alitoa wito kwa wakulima, viongozi wa serikali, ushirika na sekta binafsi kuwa na mshikamano ili kutatua tatizo la sukari.

Aidha, alikemea vitendo visivyo vya uadilifu vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika na kusababisha migogoro.

"Hakuna kiongozi wa ushirika atakayekula hela ya mkulima akabaki salama," alisisitiza Waziri Bashe.

Aliwataka viongozi hao kufanya kazi kwa weledi ili wakulima wapate haki zao za msingi.

# Makalla awaonya wavamizi viwanja

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewaonya wananchi wanaovamia maeneo ya taasisi na watu binafsi na kujenga kuwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria.

Alitoa onyo hilo katika kikao kilichojumuisha wakuu wa wilaya, kamati za ulinzi na usalama, wakurugenzi, wastahiki meya, makatibu tawala, wenyeviti wa mitaa, watendaji wa kata/ mitaa na kusisitiza serikali haitowafumbia macho wavamizi hao.

Pia aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi kusikiliza na kutatua tatizo la migogoro ya ardhi.

Aliagiza taasisi na wananchi kuyalinda na kuyaendeleza maeneo yao ili yasivamiwe huku akiwataka wananchi kujiridhisha na nyaraka na taarifa za Serikali ya Mtaa kabla ya kununua eneo.

Katika hatua nyingine, Makalla ametangaza operesheni ya usafi wa barabara kuu za mkoa huo ifikapo Jumamosi ya Julai 30 na kuagiza wananchi na makandarasi wa kampuni za uzoaji wa taka kushiriki kwenye usafi huo.

Katika kikao kazi kilichojumuisha viongozi wa ngazi ya wilaya, kata, mitaa na wadau mbalimbali wa maendeleo, Makalla alisema Jiji la Dar es Salaam lina uwezo wa kutoka kwenye nafasi ya sita kwa usafi barani Afrika na kushika nafasi za juu.

Aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuitisha kikao na watendaji wa kata na mitaa kabla ya Julai 30 ili kuweka mipango.

Katika operesheni hiyo, alitaka ufanyike usafi wa mito na maboresho ya fukwe huku akiwataka makandarasi wa uzoaji wa taka zinazokusanywa ziondolewa kwa wakati.

Miongoni mwa barabara kubwa ambazo RC Makalla ameelekeza kufanyiwa usafi ni Barabara ya Nyerere, Bagamoyo, Morogoro, Mandela, Kilwa na Pugu.

halopesa *150*88#

## Ada za wateja

| Kiwango (TSH) | | Customer fee (TSH) | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kwenda HaloPesa | | | Kwenda mitandao mingine | | | Tuma kwa namba isiyosajiliwa | | | Kutoa pesa | | |
| Kutoka | Mpaka | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato |
| 100 | 999 | 10 | 10 | 20 | 10 | 10 | 20 | - | 10 | 10 | - | 10 | N/A |
| 1,000 | 1,999 | 20 | 10 | 30 | 32 | 10 | 42 | 350 | 10 | 360 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 20 | 10 | 30 | 32 | 10 | 42 | 380 | 10 | 390 | 300 | 10 | 310 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 15 | 65 | 63 | 15 | 78 | 475 | 15 | 490 | 400 | 15 | 415 |
| 4,000 | 4,999 | 55 | 30 | 85 | 77 | 30 | 107 | 530 | 30 | 560 | 500 | 30 | 530 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 60 | 190 | 162 | 60 | 222 | 710 | 60 | 770 | 780 | 60 | 840 |
| 7,000 | 9,999 | 130 | 70 | 200 | 162 | 70 | 232 | 790 | 70 | 860 | 780 | 70 | 850 |
| 10,000 | 14,999 | 320 | 128 | 448 | 450 | 128 | 578 | 1,250 | 128 | 1,378 | 1,200 | 128 | 1,328 |
| 15,000 | 19,999 | 320 | 243 | 563 | 450 | 243 | 693 | 1,250 | 243 | 1,493 | 1,200 | 243 | 1,443 |
| 20,000 | 29,999 | 360 | 383 | 743 | 495 | 383 | 878 | 1,550 | 383 | 1,933 | 1,500 | 383 | 1,883 |
| 30,000 | 39,999 | 370 | 439 | 809 | 558 | 439 | 997 | 1,620 | 439 | 2,059 | 1,600 | 439 | 2,039 |
| 40,000 | 49,999 | 380 | 599 | 979 | 648 | 599 | 1,247 | 1,800 | 599 | 2,399 | 2,100 | 599 | 2,699 |
| 50,000 | 99,999 | 580 | 818 | 1,398 | 900 | 818 | 1,718 | 2,350 | 818 | 3,168 | 2,500 | 818 | 3,318 |
| 100,000 | 199,999 | 700 | 1,009 | 1,709 | 1,350 | 1,009 | 2,359 | 2,750 | 1,009 | 3,759 | 3,300 | 1,009 | 4,309 |
| 200,000 | 299,999 | 750 | 1,173 | 1,923 | 1,620 | 1,173 | 2,793 | 4,200 | 1,173 | 5,373 | 4,500 | 1,173 | 5,673 |
| 300,000 | 399,999 | 950 | 1,397 | 2,347 | 1,800 | 1,397 | 3,197 | 5,600 | 1,397 | 6,997 | 5,500 | 1,397 | 6,897 |
| 400,000 | 499,999 | 1,200 | 1,636 | 2,836 | 1,980 | 1,636 | 3,616 | 6,600 | 1,636 | 8,236 | 6,000 | 1,636 | 7,636 |
| 500,000 | 599,999 | 1,300 | 2,075 | 3,375 | 2,520 | 2,075 | 4,595 | 7,500 | 2,075 | 9,575 | 6,400 | 2,075 | 8,475 |
| 600,000 | 699,999 | 1,400 | 2,554 | 3,954 | 2,880 | 2,554 | 5,434 | 7,600 | 2,554 | 10,154 | 7,000 | 2,554 | 9,554 |
| 700,000 | 799,999 | 1,400 | 2,833 | 4,233 | 2,880 | 2,833 | 5,713 | 7,650 | 2,833 | 10,483 | 7,000 | 2,833 | 9,833 |
| 800,000 | 899,999 | 1,750 | 3,000 | 4,750 | 3,150 | 3,000 | 6,150 | 8,100 | 3,000 | 11,100 | 7,500 | 3,000 | 10,500 |
| 900,000 | 1,000,000 | 1,750 | 3,551 | 5,301 | 3,150 | 3,551 | 6,701 | 8,300 | 3,551 | 11,851 | 7,500 | 3,551 | 11,051 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 3,000 | 3,751 | 6,751 | 3,600 | 3,751 | 7,351 | 8,300 | 3,751 | 12,051 | 7,500 | 3,751 | 11,251 |
| Above 3,000,000 | | 3,000 | 4,000 | 7,000 | 4,500 | 4,000 | 8,500 | 8,300 | 4,000 | 12,300 | 7,500 | 4,000 | 11,500 |

216949701

# Watanzania watangaziwa fursa kozi fani za tiba India

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha CT cha nchini India, kimewashauri wanafunzi wa Kitanzania kuchangamkia kozi za tiba zisizo za udaktari ambazo zinatolewa kwa gharama nafuu kwenye chuo hicho.

Chuo hicho kimetangaza punguzo la asilimia 50 kwa wanafunzi Watanzania watakaodahiliwa kwenda kusoma kwenye chuo hicho ikiwa ni motisha ya kwa wengine kujiunga na fani hizo.

Hayo yalisemwa jana Naibu Mkurugenzi wa chuo hicho, Gaurav Sharma, kwenye maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea jijini Dar es Salaam, vikiwamo 10 kutoka nje ya nchi vinavyoshiriki kupitia mwamvuli wa Global Education Link (GEL).

Alisema wanafunzi wengi wa Tanzania wanachangamkia mafunzo hayo kutokana na soko lake kubwa kwenye nchi mbalimbali duniani kwa sasa kuna wanafunzi 100 wa Tanzania wanaosoma kwenye chuo hicho.

Alitaja kozi zinazofundishwa kuwa ni ufamasia, taaluma ya usingizi, teknolojia ya maabara, mionzi, teknolojia ya chumba cha upasuaji, physiotherapy (mamacheza) na Shahada ya Afya ya Jamii.

Alisema nchi nyingi duniani zinakabiliwa na upungufu wa wataalamu wa usingizi, mionzi na wale wa teknolojia inayotumika kwenye vyumba vya upasuaji na chuo hicho kimekuwa kikitoa wataalamu wengi kutoka mataifa mbalimbali.

Alisema Chuo cha CT pia kimekuwa kikitoa wataalamu wa fani za akili bandia (artificial intelligence) na teknolojia ya hali ya juu kwa watu wanaofanyiwa matibabu ya moyo.

Alisema pia kimekuwa kikizalisha wataalamu wa kuhudumia wagonjwa mahututi na namna ya kuwahudumia wagonjwa wanaohitaji kuchujwa au kubadilishwa damu (Dialysis).

Mkurugenzi wa GEL, Abdulmalik Mollel, alisema wanafunzi wanaokwenda kusoma kwenye vyuo vya nje wanachota ujuzi na kurejea kusaidia taifa lao kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema zamani wazazi waliogopa kuruhusu watoto wao kwenda nje ya nchi kusoma wakidhani hawatarejea, lakini wengi wamekuwa wakichukua ujuzi na kuja kuutumia nyumbani.

"Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo vikuu wanapaswa kutembelea mabanda ya Global Education Link kwenye maonyesho ya Mnazi Mmoja kwasababu kuna uwakilishi wa vyuo 10 kutoka nje ambao watawaeleza kuhusu kozi wanazotoa na wataalamu wetu watawapa taarifa ili wawe na chaguo sahihi," alisema.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya uongozi na uchumi wa mwanamke mkoani Iringa wakiwa katika mafunzo yaliyoandaliwa na taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Star Woman Foundation jana kwenye Ukumbi wa Siasa ni Kilimo Iringa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# BAKWATA kushirikiana na Polisi kukomesha ukatili wa kijinsia

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Singida, limeweka mkakati wa kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa ajili ya kukomesha vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia, ulawiti na ubakaji katika mkoa huo.

Shekhe wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, akizungumza juzi katika usiku wa Stara, alisema maadili yamezidi kuporomoka katika mkoa huo na kuufanya kuwa wa kwanza katika matukio ya unyanyasaji wa kijinsia.

"Takwimu zinaonyesha masuala ya unyanyasaji wa kijinsia, ulawiti na biashara ya binadamu mkoa wetu umetajwa kuongoza, hili sio jambo jema inauletea sifa mbaya mkoa wetu," alisema.

Shekhe Nassoro alidai hivi sasa kumeibuka matukio ya ubakaji kuanzia saa 11:00 hadi 12:00 jioni kwa baadhi ya madereva wa bajaji kudaiwa kubaka wanawake na watoto wanapowachukua kama abiria kwenye vyombo vyao vya usafiri. Alisema kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo BAKWATA inashirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha matukio hayo yanakomeshwa na kuna kitengo cha kushughulikia masuala ya kijinsia katika ofisi ya Shekhe wa Mkoa.

Aidha, Shekhe Nassoro alitangaza kupiga marufuku watoto kusafirishwa kwenda nje ya mkoa huo kwa ajili ya kufanya kazi za ndani kutokana na vitendo hivyo kuchochea matukio ya unyanyasaji wa kijinsia. "Hivi sasa tumeweka utaratibu mtoto yeyote anayesafirishwa kutoka Singida kwenda mikoa mingine au nje nchi ni lazima atambulishwe kupitia ofisi ya BAKWATA mkoa ili kutunza taarifa zake ili hata akipata changamoto yoyote anasaidiwa," alisema.

Naye Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi anayeshughulikia Dawati la Jinsia, Damas Mwakisabwe, alisema matukio ya kulawiti, ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia yamekuwa janga kubwa katika mkoa huo.

Mwakisabwe alisema matukio hayo yanatokea kutokana na wazazi kusahau majukumu yao ya kuwalea watoto wao katika maadili na kusababisha kujiingiza katika vitendo vibaya.

"Zipo kesi nyingi za matukio ya unyanyasaji wa kijinsia ambayo Jeshi la Polisi inapata na cha kushangaza matukio haya baadhi ya watoto wanafanyiwa wakati mwingine na ndugu zao wa karibu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Yusuph Mwandami, ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema kumekuwa na watoto wengi wa mitaani na kutaka viongozi wa dini kukaa upya na serikali kuangalia sheria ya ndoa ili ifanyiwe marekebisho.

"Hili ongezeko la watoto wa mitaani ni changamoto na linasababishwa kuwapo kwa ongezeko la wanandoa yaani baba na mama kuachana na hivyo watoto kukosa mlezi," alisema.

## RC awashukia waliochukua mikopo 10% kurejesha

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, ameagiza vikundi vilivyochukua mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwa ajili ya vijana, wanawake na wenye ulemavu na kuhama mkoa huo kujisalimisha ili vipewe utaratibu wa kuanza kulipa deni hilo.

Vikundi hivyo vinadaiwa kuchukua mikopo hiyo miaka mitatu iliyopita na kuhama mkoa huo.

Alisema vikundi mbalimbali vya mkoa huo Mwanza vilikopa fedha na kushindwa kurejesha zaidi ya Sh. bilioni 4.9 kwa miaka mitatu na kwamba baada ya kuanza operesheni maalumu ya kutaka zirudi zimerejeshwa Sh. bilioni 1.4 mpaka kufikia jana.

Aliongeza fedha hizo kurudishwa baada ya kuagiza kamati za ulinzi na usalama kuanza kufanya kazi ya kuzitafuta ili kusaidia watu wengine.

Kazi ya kusaka fedha hizo ilifanyika kwa miezi mitano iliyopita na zimerudi katika mfuko wa halmashauri zote mkoani Mwanza.

"Vikundi vingi vya vijana, wanawake na wenye ulemavu vilichukua fedha za halmashauri kama mkopo na vingine kuamua kuhama mkoa, nataka sasa vije tuanze kuzungumza navyo ili kuona namna ya kuanza kulipa ili ziwafaidishe watu wengine," alisema Gabriel.

Alisema fedha hizo ni kwa ajili ya watu ambao wanataka kuanzisha miradi ili wajikomboe kimaisha na sio kuwakopesha watu wenye ajira.

Alisema mkanganyiko huo umeleta shida ambayo imesababisha watu wengine wakiwamo watumishi wa halmashauri kukopa fedha hizo wakati hawastahili.

Mkuu huyo wa mkoa alisisitiza fedha za halmashauri zinazotengwa ni kwa ajili ya makundi ya vijana, wenye ulemavu na wanawake na kwamba mtu mwingine hatakiwi kuingia.

Aidha, Gabriel aliwaonya wanaokopeshwa fedha na kisha wakiondoka eneo la benki wanagawana na kuziweka mifukoni mwao badala ya kuzipeleka katika miradi.

Alisema hatua hiyo ni hatari kwa kuwa fedha za halmashauri zitakuwa zinatengwa kila mwaka na kuishia katika mifuko ya watu badala ya kusaidia makundi yaliyokusudiwa.

Licha ya ulipaji wa mikopo hiyo kusuasua, Mkuu wa Mkoa jana alitangaza kuanza tena mchakato wa kukopesha fedha hizo kwa vikundi ambavyo vimekidhi vigezo.

Alisema mwaka huu halmashauri zote mkoani Mwanza zimetenga Sh. bilioni 2.3 na kuwataka vijana, wanawake na wenye ulemavu wazichangamkie ili ziweze kuwasaidia kuanzisha na kuendeleza miradi yao.

# Askari, Mtendaji mbaroni tuhuma za rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

ASKARI polisi Juma Manyama na Mtendaji wa Kijiji cha Lulembela, wilayani Mbogwe, Maulidi Kayege wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bukombe Mkoa wa Geita makosa ya tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 42,000.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Ainawi Moshi, ilidaiwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Husna Kiboko, kuwa watuhumiwa hao walitenda makosa hayo Januari 3, mwaka 2021.

Alidai kuwa washtakiwa hao wanadaiwa kupokea rushwa ya Sh. 42,000 kutoka kwa Stefano Magembe, kupitia kwa Kamori Dickson kama ushawishi ili wasichukuliwe hatua za kisheria kwa kosa la kusafirisha mbao bila kibali.

Wakili huyo alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali.

Hakimu Moshi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Julai 28, mwaka huu, kwa ajili ya kuwasomea maelezo ya awali.

Aidha, Hakimu Moshi alisema masharti ya dhamana yako wazi kwa kila mshtakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika Sh. 100,000 kwa kila mdhamini.

Washtakiwa wote kwa pamoja walitimiza masharti ya dhamana na wako nje kwa dhamana.

# Mapenzi, uchumi chanzo cha matatizo ya akili

**Na Joseph Mwendapole**

MATATIZO ya kiuchumi na uhusiano wa kimapenzi vimetajwa kuongoza katika visababishi vya matatizo ya afya ya akili.

Hayo yalisemwa jana na Mkufunzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii ya Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki (HKMU), Esther Katende, wakati akizungumzia kambi ya mwezi mmoja iliyoandaliwa na chuo hicho kupima afya ya akili jijini Dar es Salaam.

Alisema mpaka mwishoni mwa wiki iliyopita walikuwa wamewapima na kuwapa ushauri zaidi ya watu 200, huku magonjwa ya shinikizo la damu na kisukari yakionekana kutesa watu wengi.

"Watu wengi waliokuwa wakipata ushauri baada ya kuhojiwa ilionekana wanamatatizo ya afya ya akili kutokana na maelezo waliyoyatoa wenyewe kisababishi kikuu kilionekana kuwa ni matatizo ya uchumi na mahusiano," alisema.

Alisema Watanzania wengi wanaamini kuwa mtu mwenye tatizo la afya ya akili ni kichaa anayeokota makopo au kutembea bila nguo, dhana ambayo siyo sahihi kwani kuna wanaovaa vizuri lakini wana matatizo ya afya ya akili.

"Msongo wa mawazo unaweza kusababisha ukawa na shida kwenye afya ya akili na ndiyo sababu watu wanachukua maamuzi yasiyo mazuri kutokana na msongo mkubwa wa mawazo," alifafanua Esther.

Aidha, alisema waliamua kuandaa mwezi wa afya ya akili baada ya kuona tatizo linaongezeka na matukio mengi ya mauaji yanazidi kushamiri sehemu mbalimbali nchini.

Alisema pia wanapima afya kwa ujumla kwa watu wote watakaojitokeza kwenye kambi hiyo na kuwapa ushauri wa kitaalamu wale watakaokutwa na shida mbalimbali.

Viashiria vya tatizo la afya ya akili viko vingi, mojawapo ni kujitenga au kutengwa, ukimya usio wa kawaida, mabadiliko katika mtiririko wa mawazo, maongezi na matendo ya mhusika.

"Idara ya Ustawi wa Jamii ya Hubert Kairuki Memorial University pamoja na vyuo vingine vinavyotoa elimu ya Ustawi wa Jamii ni chimbuko mojawapo la wataalamu wanaotoa huduma kwa wagonjwa wa aina hiyo," alibainisha Esther.

Katika Siku ya Afya ya Akili mwaka jana, Shirika la Afya Dunia (WHO), lilisema mzigo wa matatizo ya akili miongoni mwa vijana balehe unasababisha mambo makubwa matatu ambayo ni msongo wa mawazo na kujiua.

Ilisema kujiua kutokana na msongo wa mawazo ni sababu inayoshika nafasi ya pili kwa vifo vya vijana kati ya umri wa mika 15-19 na tatizo linaloongoza ni matumizi mabaya ya pombe na mihadarati.

WHO ilisema hali hiyo inafanya matatizo ya akili kuwa moja ya changamoto kubwa kwa nchi nyingi duniani na huchangia kuwaweka vijana kwenye hatari kama ya kufanya ngono isiyo salama, na hata uendeshaji mbovu wa magari unaosababisha vifo vya vijana wengi. Ilisema athari za kutoshughulikia matatizo ya afya ya akili kwa vijana ni kubwa mara nyingi zinaendelea hadi ukubwani na kuwakosesha fursa ya kushamiri katika maisha yao.

Naye Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, katika ujumbe wake wa siku ya afya ya akili mwaka jana alisisitiza umuhimu wa serikali kuwekeza zaidi kwenye sekta za afya, elimu na jamii katika kudhibiti janga hilo.




Mwakilishi wa Chuo Kikuu cha Geomedi cha nchini Georgia, Irene Shaduri, akiwaelezea kuhusu chuo hicho wanafunzi na wazazi waliofika kwenye banda la Global Education Link (GEL) katika maonyesho ya vyuo vikuu Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kiwanda cha shayiri kufufuliwa mwakani

**Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL) imeweka wazi mkakati wake wa kukifufua kiwanda cha kuchakata shayiri cha Moshi Malting Plant kufikia mwakani ili kutoa fursa zaidi za masoko kwa wakulima wa shayiri.

Kiwanda hicho kilichosimamisha shughuli zake mwaka 2017, kitaongeza uwezo wa kuchakata kufikia takriban tani 30,000 za shayiri kwa mwaka kutoka tani 15,000 kwa mwaka ilivyokuwa awali.

Mtaalamu wa Kilimo wa TBL, Joel Msechu, alibainisha hayo jijini hapo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakulima yaliyofanyika Kata ya Monduli Juu, Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, yakiwa na kaulimbiu 'Kilimo cha kisasa, kuboresha mnyororo wa thamani'.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na wakulima, taasisi za kifedha, kampuni za bima, maofisa ugavi huku serikali ikiwakilishwa na Ofisa Tawala Wilaya ya Monduli, Catherine Moshi, akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe.

Akizungumzia mpango wa ufufuaji wa kiwanda cha Moshi Malting Plant, Msechu alisema TBL ilisitisha shughuli za kiwanda hicho mwaka 2017 kutokana na gharama za uendeshaji, hasa kwenye matumizi ya maji na umeme kwa kuwa kilikuwa kinatumia teknolojia ya kizamani.

"Kampuni ilifikia uamuzi wa kusimamisha shughuli za kiwanda kutokana na gharama za uendeshaji kwani kiwanda kilikuwa kinatumia teknolojia ya kizamani, ila sasa kampuni iko kwenye mpango wa kukifufua kufikia mwaka kesho na kuanza shughuli za uchakataji shayiri.

"Kiwanda kitakuwa kinatumia teknolojia ya kisasa, hivyo tutaweza kuhimili gharama za uendeshaji na tutaweza kukuza uwezo wa uchakataji shayiri kutoka tani 15,000 kwa mwaka mpaka kufikia tani 30,000," alisema Msechu.

Aliongeza kuwa kiwanda kitakapoanza shughuli mwakani, kitaanza na uzalishaji wa tani 12,000 na kuendelea kuongeza uwezo kila mwaka mpaka kufikia tani 30,000.

Akizungumzia Siku ya Wakulima wa zao hilo, Msechu alisema TBL inaamini kwenye nguvu ya kujenga ushirikiano na kwa maendeleo endelevu, hivyo maadhimisho hayo ya Siku ya Wakulima ya kila mwaka, yanatoa nafasi kwa wakulima kujifunza na kupata fursa ya kuunganishwa na wadau wengine kama benki na kuangalia namna ya kuwapatia wakulima bima.

Pia, TBL imejizatiti kuwawezesha wakulima kwa kuwapatia masoko ya uhakika ya mazao yao na kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kufanya kilimo cha kisasa na endelevu kitakachowawezesha kukua zaidi na hatimaye kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye uchumi wa taifa kama ilivyoidhinishwa kwenye kampeni ya Kilimo Ajenda 10/30 ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Ofisa Tawala Wilaya ya Monduli, Catherine Moshi, alisema serikali imejizatiti kukuza na kuboresha sekta ya kilimo kwenye uchumi na hatimaye kuongeza mchango wa sekta hii kwenye mapato ya serikali.

"Wakati serikali inaendelea kuchukua hatua za kimkakati za kuboresha sekta ya kilimo, tunafarijika kuona wadau wengine kama TBL nao wakichukua hatua stahiki kwa lengo la kukuza sekta hii, hivyo serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa wadau hawa," alisema.

Aliongeza kuwa kukuza uzalishaji wa shayiri na sekta ya kilimo kwa ujumla ni kipaumbele kwa serikali na ndiyo maana hivi karibuni serikali ilizindua kampeni ya Kilimo Ajenda 10/30 ikiwa ni mpango wa kuboresha sekta hii na mchango wake kwenye uchumi.

Mwaka jana maadhimisho ya siku ya wakulima yalijikita kwa wakulima wa zabibu na kuainisha mafanikio makubwa kwa wakulima wa zabibu na kuingizwa rasmi kwenye kilimo cha kimkataba na TBL kwa lengo la kukuza kilimo cha zao la zabibu ili kuchangia uzalishaji endelevu wa zabibu nchini.

# WanaCCM waonywa makundi kuelekea uchaguzi Oktoba

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetoa onyo kwa wanachama waliojitokeza kuchukua fomu kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho kuacha kutengeneza makundi na kufanya kampeni kabla ya wakati.

Onyo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu wa chama hicho Wilaya ya Masasi, ambaye ni Mkurugenzi wa uchaguzi wilaya hiyo, Didas Zimbihile, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa CCM, Oktoba mwaka huu.

Alisema hamasa ya wanachama kuchukua fomu za kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi wa Oktoba 2022 ndani ya CCM imekuwa kubwa ikilinganishwa na chaguzi zilizopita katika wilaya hiyo.

Alisema hadi Julai 13, dirisha la urejeshaji fomu likifungwa jumla ya wanachama 153 walijitokeza kuchukua fomu na tayari wote wamerejesha wakisubiri hatua ya mchujo.

Katika nafasi ya uenyekiti waliojitokeza kuomba ni 15 kati ya hao wanawake ni wawili na wote wamesharejesha fomu.

Zimbihile alisema nafasi nyingine ya juu na nyeti ndani ya chama hicho ambayo pia imevunja rekodi kwa kujitokeza idadi kubwa ya wanachama kuomba ya katibu wa siasa na uenezi wilaya ambayo wanachama 18 kati ya hao wanawake ni watatu pekee.

Nafasi nyingine iliyokuwa na idadi kubwa ya wanachama kuchukua fomu ni ujumbe wa halmashauri kuu wilaya.

"Katika uchaguzi huu wanachama wamehamasika sana kujitokeza kugombea nafasi za uongozi na hapa tunatoa onyo kwa wanachama hawa kuacha kutengeneza makundi na kufanya kampeni mapema," alisema Zimbihile.

Mwitikio huo wa wanachama kujitokeza kugombea, alisema umekuja baada ya chama hicho mapema mwaka huu kuendesha semina ya kuhamasisha wanachama wake kugombea nafasi za uongozi.

Pia, katika kuelekea uchaguzi ndani ya chama mwezi Oktoba, kimetoa onyo kwa wanachama waliojitokeza kugombea kutotengeneza makundi na kuacha kufanya kampeni kabla ya wakati.

Alisema atakayebainika kufanya kampeni nje ya wakati chama kitamchukulia hatua ikiwamo kumwondoa katika fursa ya kugombea kwa kuwa atakuwa amevunja kanuni na taratibu za uchaguzi.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (katikati), akizungumza na mmoja wa wateja wapya wa benki hiyo kwenye hafla fupi ya kuwakaribisha wateja wa iliyokuwa Benki ya FNB Tanzania waliohamia Benki ya Exim, kutokana na benki hiyo kuinunua ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wake wa kujitanua zaidi ndani na nje ya mipaka ya nchi. Hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge amwangukia Waziri Mkuu jimbo lisichukuliwe

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MBUNGE wa Iramba Mashariki, Francis Izack, amehofu kupata upinzani katika uchaguzi mkuu 2025 kutokana na wapinzani wake kuanza kulinyemelea jimbo lake mapema wakitumia hoja ya kutojengwa barabara ya lami inayounganisha makao makuu ya Wilaya ya Mkalama.

Kutokana na hali hiyo, amemwomba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amwokoe ijengwe barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 42 kutoka Iguguno inapopita barabara kuu ya Singida-Mwanza hadi katika Kijiji cha Nduguti, yalipo makao makuu ya wilaya.

Wilaya ya Mkalama ni mpya iliyoanzishwa miaka 10 iliyopita ambayo ilimegwa kutokana na Wilaya ya Iramba barabara inayounganisha wilaya hiyo ni ya vumbi na wananchi wamekuwa wakiomba serikali ijenge barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

"Waziri Mkuu kutojengwa kwa barabara ya Iguguno-Nduguti watu wameanza kudandia jimbo, naomba uniokoe," alisema.

Nao wabunge wa Viti Maalum, Ayisharose Mattembe, Jesca Kishoa na Martha Gwau, waliungana na mbunge Isack kumwomba Waziri Mkuu ijengwe barabara hiyo kwa lami kwa kuwa imekuwa kero kubwa kwa wananchi.

Walisema barabara hiyo ni muhimu kutokana na umri wa miaka 10 wa wilaya hiyo kutosha kuiunganisha kuwa barabara ya lami ambayo itarahisisha huduma za usafiri na kuwawezesha wananchi kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko.

Waziri Mkuu, Majaliwa akijibu ombi hilo alisema suala la ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ipo kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuhakikisha itajengwa.

Majaliwa alisema kazi iliyokuwa inafanywa na serikali ni ujenzi wa barabara kuunganisha mkoa kwa mkoa ambayo imefanikiwa kwa asilimia 99 na sasa kazi inahamia kuunganisha wilaya kwa wilaya kwa kujenga barabara kwa lami.

Alisema barabara ya kutokana Iguguno hadi Nduguti yalipo makao makuu ya Wilaya ya Mkalama, upembuzi yakinifu ulishafanyika na muda si mrefu itatangazwa kwa ajili ya kuanza kujengwa.

"Mkalama mji muhimu wa kiuchumi kwa jinsi tukivyojipanga serikali hatutawaacha, wilaya hii itaendelea kujengwa hatua kwa hatua, lakini na nyie mjipange hapa ni mahali pa biashara," alisema.

Kwa upande wake Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Ndugange, alisema serikali imeongezea bajeti ya ujenzi wa barabara Wilaya ya Mkalama kutoka Sh. milioni 600 hadi Sh. bilioni 2.2 kwa mwaka huu wa fedha.

## Gwajima akiagiza kikosi kazi kurudi kwa wadau maoni sera ya jinsia

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amekitaka kikosi kazi kinachopitia Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia kurudi kwa wadau ili kupokea maoni zaidi.

Alisema hayo wakati akipokea taarifa ya kikosi kazi hicho, katika ofisi mdogo ya wizara hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, huku akikipongeza kwa kazi iliyofanyika.

Dk. Gwajima aliongozana na Naibu wake Mwanaidi Ali Khamis, Katibu Mkuu, Dk. Zainab Chaula, Naibu Katibu Mkuu, Dk. Amon Mpanju na baadhi ya wataalamu wa wizara hiyo.

Alisema, pamoja na pongezi hizo, ipo haja ya kupokea maoni zaidi kwa wadau mbalimbali wa makundi yote stahiki wakiwamo wanaume, kwa kuwa ili sera hiyo iwe na maana, ni muhimu kuwafikia wadau wote watoe maoni yao kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya jamii, kwa wakati wa sasa.

Akichangia mada baada ya wasilisho hilo lililotolewa na mtaalamu elekezi, Profesa Linda Mhando, kutoka kampuni ya Interfiri Ltd, Dk. Gwajima alisema sera itakuwa na maana iwapo hayo yatafanyika.

"Tunapoandaa sera hii, ni lazima tuoainishe na wizara nyingine mtambuka, mathalani wizara inayoshughulikia masuala ya vijana, ambayo kwa sasa ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu," alisema Dk. Gwajima.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mwanaidi Ali Khamis, akichangia katika wasilisho hilo, alisema kuna umuhimu wa kutumia wadau mbalimbali wenye uwezo kutoa mawazo ya kitaalamu katika zoezi la kuwezesha ukusanyaji wa maoni kwa haraka.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema ni muhimu kuangalia asasi za kiraia ili kila mwenye maoni ya kuboresha aweze kuingiza katika sera kwa lengo la kukidhi mahitaji ya taifa.

Mwishoni mwa Juni mwaka huu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, aliunda kikosi kazi cha watu sita 10 kilichokuwa kikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jinsia, Grace Mwangwa ili kupitia sera hiyo ya mwaka 2000.





Ukurasa 13

Ukatili kwa binadamu umeumiza pia mazingira

Nipashe
TESA
Jumanne Julai 19, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

Yanayoonyesha kuwa hata sasa misitu ni mali kwa taifa

TEKNOLOJIA
NA GERALD KITABU, TABORA

# Utafiti TARI, Brazil waleta kisasa kilimo cha pamba

• Wakulima kupata tani 1.2 kwa ekari siyo kilo 200

UNAJULIKANA kama Cotton Victoria, huu ni mradi wa ushirikiano wa watafiti wa Wizara ya Kilimo na Serikali ya Brazil, unaolenga kuongeza uzalishaji, tija na fedha kwa mkulima wa chini, anayelima pamba.

Unamlenga mkulima huyu ambaye licha ya kusota juani na kwenye mvua, kwa gharama kubwa anaambulia kilo 200 za pamba kwa ekari, ukitaka kumpandishia ili avune zaidi ya kilo 1,000.

Ni kazi inayofanyika katika kituo cha utafiti wa kilimo Ukiriguru (TARI Ukiriguru) kilichoko Mwanza, majaribio yakifanyika mikoani Mwanza, Simiyu, Geita, Shinyanga, Mara, Tabora na Katavi. Yote yanaonyesha mafanikio hasa kuwavuta wakulima kuuaga umaskini.

Mratibu wa Pamba Kitaifa, Dk. Paul Saidia, kutoka TARI-Ukiriguru, anasema katika miaka ya hivi karibuni uzalishaji na tija ya pamba umeshuka kutokana na sababu mbalimbali mojawapo ikiwa ni wadudu waharibifu, wakulima kutofuata kanuni bora za kilimo cha zao hilo na ukame.

Akitolea mfano Dk. Saidia ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti cha TARI Ukiriguru, anasema upandaji uliozoeleka zamani ni umbali kati ya mstari na mstari kuwa ni sentimita 90 na kutoka shimo hadi shimo ni sentimita 40, umbali huo umempunguzia sana mkulima tija.



Mkulima wa pamba 'dhahabu nyeupe' akijivunia mavuno. **PICHA: MTANDAO**

Anasema zamani, wakulima walipanda pamba umbali wa sentimita 90 kutoka mstari mmoja hadi mwingine halafu sentimita 40 kutoka mche hadi mche upandaji ukijulikana kama 90/40 na kupata mimea 22,222 kwa ekari moja hali iliyowawapunguzia mapato mara nne zaidi.

Anafafanua kuwa utafiti wa Brazil na Tanzania, umeboresha na kuanzia sasa wanapanda umbali wa sentimita 60 kutoka mstari mmoja hadi mwingine halafu sentimita 30 kutoka mche hadi mche 60/30 na kupata mimea pamba 44,444 kwa ekari moja.

"Ningependa kuwashauri wakulima wa pamba kote nchini kuhakikisha wanaachana na utaratibu wa zamani na waingie katika utaalamu mpya na wenye tija kwa kutumia 60/30 ambao unatoa mazao mengi." Anasema mtafiti huyo.

Dokta Saidia anatahadharisha wakulima kuwa tija inaweza kufikiwa tu iwapo utaratibu huu mpya utaambatana na wakulima kufuata kanuni bora za kilimo.

Anasema kwa kutumia mbegu zilizofanyiwa utafiti kituoni hapo za UKM 08, mkulima ana matumaini ya kuvuna zaidi ya kilo 1,000 kwa ekari iwapo atafuata kanuni bora za kilimo na upandaji uliotolewa na mradi huo.

Kupitia Cotton Victoria 2016 watafiti kutoka Ukiriguru na Brazil na Bodi ya Pamba, walifanya utafiti na kubaini kuwa wakulima wanahitaji upandaji mpya ili mkulima apate tija.

"Baada ya kujiridhisha, walianza kuwabadilisha wakulima wa mkoa wa Mwanza, walioshiriki mafunzo hayo walitoa ushuhuda wa kuongeza tija kutoka kilo 200 za awali mpaka kilo kati ya 800 na 1,200 kwa ekari. Hali hiyo iliwafanya watafiti kusambaza upandaji mpya katika mikoa ya Geita na Simiyu," anasema.

Anaongeza kuwa baada ya kubaini hilo, watafiti waliwaleta pamoja wagani kutoka kila mkoa kwa mafunzo ili nao waende kufundisha wakulima katika maeneo yao.

Wakitoa ushuhuda siku ya wakulima (farmers field day), wakulima kadhaa wa wilayani Igunga mkoani Tabora wanasema wamezoea kuvuna haba ni kati ya kilo 200 hadi 300 kwa ekari, lakini baada ya kuanza mradi huo wanapata kuanzia kilo 750 mpaka tani moja kwa ekari.

**BRAZIL NA TANI 3**

Akitoa uzoefu wa jinsi Brazil ilivyopiga hatua katika kilimo cha pamba kwa kutumia utaratibu huo mpya wa upandaji, mwakilishi wa ubalozi wa Brazil nchini William Shauri, anasema wakulima wa Brazil wanavuna kati ya kilo 2,000 na 3,000 kwa ekari.

"Hii ndiyo sababu watafiti wa Tanzania na Brazil walikutana ili kueneza mradi huu hapa nchini ambao umeleta tija kubwa kwa Brazil na kuifanya kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha pamba kwa wingi duniani," anasema.

Anasema wakulima wakiweza kupata kuanzia kilo 2,000 kwa ekari wataweza kuongeza kipato chao mara dufu na kuboresha maisha yao.

Mwakilishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dk. Deogratias Lwezaura, anatoa wito kwa wakulima na wadau mbalimbali kutumia vituo vya TARI kujipatia teknolojia rahisi na bora kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija.

ELIMU

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

# Yanayoonyesha kuwa hata sasa misitu ni mali kwa taifa

PENGINE umewahi kujiuliza ni nini maana ya kusema "miti au misitu ni mali? Inawezekana ulipata jibu au hukufahamu umuhimu wa miti au misitu kwa binadamu anayeishi katika dunia ya leo.

Heshima hiyo kwa misitu inatokana na ukweli kwamba miti ni msingi na sekta zote, inagusa sana maeneo kadhaa yanayohusu maisha ya wanadamu.

Ina faida lukuki kiuchumi kwa kuzingatia dhana ya 'miti au misitu ni mali'. Hebu sasa tuchunguze kwa undani nini kinajiri kati ya misitu na uchumi inakuwaje mali kwenye eneo hilo.

Baadhi ya mataifa au watu, uchumi wao umejikita sana katika sekta ya misitu, kwa mfano, nchi za ukanda wa 'Skandinavia' barani Ulaya kama Finland, kwa miaka mingi kabla ya mapinduzi ya kisayansi na teknolojia; uchumi wake ulitegemea sana mazao ya misitu.

Sehemu kubwa ya mapato yao yalitokana na kuuza mazao ya misitu yalioongezwa thamani kama karatasi, na bidhaa zinazojulikana kama 'engineered wood products' (EWPs) kama 'marine-boards', 'flush-doors', plywood na particle boards.'

Tanzania kwa kiasi kikubwa bado inategemea sana kuuza mbao na bidhaa za misitu ambazo hazijaongezewa thamani kikamilifu. Mathalani, kiwanda cha kutengeneza karatasi kilichoko Mgololo, wilayani Mufindi bado kinauza 'craft-paper' ambazo ni malighafi za kutengeneza vifungashi.

Aina hii ya zao la miti sasa inatumika sehemu nyingi nchini kama mifuko ya karatasi kufungashia na kubebea bidhaa mbalimbali.

Kwa mfano kwa wanaopata huduma za matibabu hivi karibuni katika baadhi ya hospitali zimetengeneza mifuko ya karatasi yenye ujazo mbalimbali kwa ajili ya wagonjwa kubebea dawa.

Mwaka 2007, ilipofika Julai baada ya Sheria ya Misitu (Cap323 RE:2002) iliyopiga marufuku kusafirisha magogo kuanza kutumika, kabla ya hapo yalikuwa yakiuzwa kama malighafi kwa viwanda vya nje.

Wafanyabiashara wa mazao ya misitu katika sekta binafsi, waliochangamkia biashara hiyo walinufaika kwa kiasi kikubwa ingawa siyo sana iwapo wangeuza



Magogo kutoka shamba la Sao Hill Mafinga huchakatwa mbao zinazouzwa soko la ndani na nje.
**PICHA: MTANDAO**

> "Kama taifa lingezalisha karatasi hapa nchini lingeokoa fedha nyingi na pengine nyingine zingeuzwa nchi za nje kupata fedha za kigeni kutunisha mfuko wa taifa.

bidhaa zilizoongezwa thamani kama samani au karatasi ngumu na laini mapato yangekuwa zaidi kwao na kwa taifa.

Baada ya kuzuia magogo na mkaa visisafirishwe nje ya nchi, baadhi waliendelea kufanya hivyo kwa kutumia njia haramu kwa kukiuka sheria na maadili dhidi ya taifa lao, nguvu kubwa iliendelea kupambana na changamoto za kupeleka magogo na mkaa nje ya nchi na hata sasa wapo wanaokazana kufanikisha lengo hilo.

Mbali na hilo, taifa miaka ya 1970, lilianzisha shamba la miti-Sao-Hill, wilayani Mufindi mkoani Iringa ili kuotesha malighafi ya kutosha kwa ajili ya kutengeneza aina mbalimbali za karatasi.

Juhudi kubwa zilifanyika na kupitia mkopo nafuu wa Benki ya Dunia (WB) wa Dola milioni 5 zikatumiwa kustawisha shamba hilo na sasa taifa linanufaika na matokeo ya juhudi hizo.

Nichukue pia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi katika vijiji vinavyozunguka shamba hilo, kwa ushirikiano wao mzuri na wenye tija kwa taifa na Watanzania wanaotumia mazao yanayotokana na bidhaa hizo.

Licha ya ukweli kwamba zimekuwapo changamoto za hapa na pale ikiwamo matukio mabaya ya kuchoma moto baadhi ya maeneo ya shamba hilo, lakini kiujumla kuna mafanikio yaliyopatikana hadi sasa. Vilevile, shamba hilo ni kielelezo kizuri kuonyesha kwamba hakika 'misitu ni mali'.

Nathubutu kusema hivyo kwa sababu 'mji wa Mafinga', wilayani Mufindi mkoani Iringa chimbuko lake ni shamba la miti la Sao-Hill. Mji huu umekua kutokana na biashara ya mazao ya miti, walianza wachache idadi imeongezeka na sana leo na sensa ya watu ya mwaka mwaka huu itafahamisha ni kwa kiasi gani wakazi wa Mafinga wameongezeka ikilinganisha na mwaka 2012. Isitoshe, hata vijiji 60 vinavyozunguka shamba ni wadau muhimu na vinanufaika.

Kwanza, kila mwaka hupatiwa takribani miche 1,000,000 ya kupanda na thamani ya mche ikiwa shilingi 300; hii ni sawa na Shilingi milioni 300 kila mwaka. Pia wamejengewa mabweni matatu ya wanafunzi wa sekondari, kwa gharama ya Shilingi milioni 350.

Kadhalika, yapo manufaa ya miundombinu na huduma za afya kwa wanavijiji na wengineo. Huu ni mfano lakini vijiji vyote vilivyo jirani na mashamba ya miti ya serikali nchi nzima wananufaika kwa namna moja au nyingine.

Nimegusia hapo juu kuhusu kiwanda cha kutengeneza karatasi kilichoko Mgololo, Mufindi. Pamoja na dhumuni la msingi la kutengeneza karatasi aina mbalimbali kwa matumizi ya kiofisi, kuchapisha magazeti na malighafi ya vifungashio, bado lengo lake muhimu halijafanikiwa. Matokeo yanayoonekana kiwanda kimejikita zaidi kwenye kuzalisha malighafi za kutengeneza vifungashio vya karatasi mifuko na maboksi. Suala la kutengeneza karatasi mbalimbali za kiofisi bado ni kitendawili.

Taifa linatumia kiasi kikubwa cha fedha za kigeni takribani dola za Marekani milioni 100 kwa mwaka kuagiza karatasi kutoka nje. Hiki siyo kiasi kidogo cha fedha ni takribani zaidi ya Sh. bilioni 23 za fedha za Tanzania.

Kama taifa lingezalisha karatasi hapa nchini lingeokoa fedha nyingi na pengine nyingine zingeuzwa nchi za nje kupata fedha za kigeni kutunisha mfuko wa taifa.

Kwa nini hatujafanikiwa kufikia hilo lengu kuu la kuanzisha kiwanda cha kutengeneza karatasi (takribani miaka 40 iliyopita) na nani alaumiwe? Ni hoja zaidi ya uwezo wangu.

Lakini, ipo nia njema na ya msingi ya kulitafakari suala hili kwa kina na kuona jinsi ya kusonga mbele bila kuathiri madhumuni ya kuanzisha kiwanda cha karatasi nchini. Hapa mchango wa sekta binafsi unatakiwa sana wakati viongozi serikalini wakiwa ndiyo machampioni wa kuhakikisha taifa linafanikiwa kwa kushirikiana na sekta binafsi ipasavyo.

Hakuna lisilowezekana iwapo wanayo dhamira kamilifu na kwa mioyo mikunjufu, wataweza kutumia rasilimali misitu kwa faida kubwa ya taifa. Misitu ni uchumi mkubwa ambao haujapewa kipaumbele cha kutosha kwa faida ya wote.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

RAI YA MAASKOFU

# Ukatili kwa binadamu umeumiza pia mazingira

• Wasisitiza kuyatunza ili kuuthamini uumbaji



Kardinal Luis Antonio Tagle, mwakilishi wa Papa Fransisko kwenye Mkutano wa AMECEA Dar es Salaam, anasisitiza kulinda mazingira. **PICHA: MTANDAO**

TANZANIA inafanya juhudi za kulinda na kutunza mazingira, mathalani, kauli mbiu ya ulinzi wa misitu inafahamika na wengi, wakikumbushwa kuwa usikate mti kabla hujapanda miti. Ndipo kinapoibuka kibwagizo kata 'mti' panda 'miti'.

Aidha, kuna kuhimiza jamii kupanda miti, kila mmoja anasisitizwa kuwa na mti nyumbani, ofisi na mitaani anapoishi ili kupata kivuli, lakini uwe mti wa matunda ili umpatie tija zaidi kivuli na matunda kwa ajili ya chakula na mengine kuuza na kupata fedha.

Kazi ya kulinda mazingira ni kila 'uumbaji' unahitaji kutunzwa, ulinzi wa maji na viumbe bahari unasisitizwa, kuharibu vyanzo vya maji kunakatazwa, aidha serikali imepiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki yanayochafua ardhi, maji na anga.

Sekta na taasisi mbalimbali zinashiriki kampeni hizo na hivi karibuni Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu Wakatoliki wa Afrika Mashariki na Kusini (AMECEA), limetangaza azma ya kutekeleza ajenda ya kulinda mazingira sambamba na uinjilishaji (kuhubiri Injili).

Kutunza mazingira ni mkakati uliopewa jina la 'Laudeto Si' Ujumbe ulio kwenye Barua ya Kichungaji ya Baba Mtakatifu Fransisco. Laudato Si ni Kiitaliano ikimaanisha kumtukuza Mungu aliye chanzo cha uumbaji au mazingira.

Hayo yanaelezwa na Mwadhama Luis Antonio Kardinali Tagle, Rais wa Baraza la Kipapa la Uinjilishaji wa Watu, anayehubiri katika Misa ya Kufungua Mkutano wa AMECEA, iliyofanyika Uwanja wa Taifa Dar es Salaam.

Kardinali Tagle anasema ukatili dhidi ya watu umeendelea hadi kuwa ukatili dhidi ya mazingira na kwamba ukosefu wa kujali, kutunza na kulinda binadamu wengine, umesababisha mazoea ya uharibifu wa uumbaji ambayo ndiyo mazingira.

Anasema ukatili huo umechangia mizozo na hata kuangamiza maisha ya watu na viumbe kama mimea, wadudu na wanyama pia wameathirika.

Waraka huo, unatolea wito makanisa na jamii kutunza mazingira kama nyumba ya kila mtu ya kuishi ili kuwe na dunia salama isiyo na hatari ya kutoweka kama ilivyo sasa.

Unalenga kushirikiana na waumini, serikali, jamii na wadau wote kuokoa mazingira kwani hewa imechafuliwa, ardhi na maji vimechafuka, miti na misitu imetoweka, lakini majira yanabadilika yanaleta joto na baridi kali, vimbunga na ukame.

Anamnukuu Papa Francis, anayeiamsha dunia akisema iko hatarini inatishiwa kuangamia kutokana na ongezeko la joto ardhini, bahari na angani, anahimizi kuipenda na kuilinda dunia kwa kuthamini kazi za uumbaji, na kutambua kuwa kila kilichoumbwa kina thamani na kimewekwa ili kumtunza na kumsaidia binadamu.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Taifa Dar es Salaam, Kardinali Tagle, anakumbusha kuwa machufuko, mauaji na ukatili dhidi ya binadamu ni matokeo ya ukatili kwa mazingira ambayo yamesababisha kuyaharibu maumbile ya asili."

Anaongeza kuwa watu wanaumizana wao kwa wao, kuwa na chuki kwenye jamii lakini wanafanya ukatili huo kwa viumbe wengine kama kukata miti, kuchoma mapori, kuua wanyama na wadudu na kuchangia kutothamini uumbaji ambayo ni mazingira au 'nyumbani kwetu', kwa vile dunia ikiharibika kila mmoja ataathirika.

Waraka wa 'Laudeto Si', unashuhudia kutoweka misitu, kuua viumbe kama samaki baharini kwa baruti, uvuvi wa sumu, kuelekeza taka za sumu kwenye maji na uzalishaji na viwanda vinavyochafua hewa angani vyote vinaiharibu dunia.

Uharibifu huo wa ikolojia umesababisha wanyama, mimea kutoweka, mito na maziwa kujaa taka kuanzia za sumu na za kila namna hasa mamilioni ya tani za plastiki ambyo ni kitisho kikubwa kwa viumbe habari.

Ni wazi kuwa anga nalo halikubaki salama limechafuka moshi na ukungu wenye sumu unaongeza joto duniani, yote haya yanaonyesha kuwa dunia inahitaji kulindwa kwa kuthamini tena uumbaji.

> AMECEA inatoa wito wa kuwa na kampeni kali na makini za kuhamasisha kulinda na kutunza (uumbaji) mazingira kuanzia chini hadi juu, ili kuongeza uelewa kwa jamii yote.

**MZOZO KIMAZINGIRA**

Wakati wa kuufunga mkutano huo wa AMECEA, Jumapili iliyopita, Mwenyekiti wa AMECEA Mhashamu Askofu Charles Kasonde, kutoka Zambia, anasoma azimio la pamoja linalotolewa baada ya mkutano huo unaowakutanisha maaskofu na wajumbe kutoka Ethiopia, Eritrea, Kenya, Malawi, Tanzania, Uganda, Sudani na Sudani ya Kusini, Zambia na wajumbe waalikwa kutoka Djibouti, Somalia, akisema wote wanathibitisha kuwapo mzozo wa kiikolojia.

Ikolojia ni maingiliano baina ya wanadamu na mazingira yao na jinsi wanavyotumia rasilimali na maliasili zilizoko. Kwa mtizamo huo, anasema viongozi hao wanaona mzozo huo unaothibitishwa na athari hasi za mabadiliko ya hali ya hewa ambayo ni ukame mkali, mafuriko, vimbunga na mvua zisizotabirika, yote yanazidi kuwa tishio kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi za ukanda Afrika Mashariki na Kusini.

"Tunasikitishwa sana na kasi ya misitu yetu kutoweka haraka kutokana na matumizi ya kuni, kuchoma mkaa na kwa shughuli za ujenzi wa makazi, viwanda na miundombinu huku kukikosekana jitihada za kutosha kupanda tena miti. Vile vile tunaona matokeo hasi ya kuchimba madini na ukosefu wa mifumo bora ya usimamizi wa taka zinazotokana na madini hayo na taka nyingine zinazozalishwa katika nchi zetu," anasema Askofu Kasonde.

Anaongeza: "Tunafahamu kwamba kushughulikia masuala haya kunagusa haki ya kiuchumi na haki nyingine, kwa hivyo, haviwezi kushughulikiwa vya kutosha bila kuzingatia ipasavyo. Kutoa njia mbadala kama vile kukuza matumizi ya nishati ya jua, upepo na bayo gasi ili watu kujipatia riziki. Hata hivyo, haya yote yanachangia uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa mazingira katika eneo la AMECEA."

AMECEA inatoa wito wa kuwa na kampeni kali na makini za kuhamasisha kulinda na kutunza (uumbaji) mazingira kuanzia chini hadi juu, ili kuongeza uelewa kwa jamii yote.

Aidha, Askofu Kasonde anasisitiza jamii kufundishwa umuhimu wa kuunganisha juhudi za kulinda mazingira na elimu kwa kufundisha ikolojia na kuanzisha mitaala na program ya kuiwezesha jamii vijana, watoto katika shule zote kufahamu umuhimu wa kulinda na kutunza ikolojia ya asilia ambao ni uhusiano bora kati ya mtu na viumbe,

INAENDELEA UK.14

# Ukatili kwa binadamu umeumiza pia mazingira

INATOKA UK.13

miti, wanyama, mimea, maji, ardhi, hewa vinavyomzunguka.

"Tunasisitiza haja ya wanachama wa AMECEA kushirikiana na serikali, madhehebu mengine, jumuiya za kidini, familia, sekta binafsi, asasi za kiraia na taasisi za maendeleo ya kijamii na kila mtu kuhamasisha utunzaji wa mazingira na kubadilisha mitazamo ya watu ili walinde maji, misitu, ardhi, wanyama, wadudu na hewa ili sote tuwe salama na dunia iwe mahali salama," anasema Mwenyekiti wa AMECEA.

**YANAHITAJIKA MATENDO**

Askofu Isaac Imani, wa Jimbo Kuu la Arusha anazungumza na Nipashe, kuhusu namna gani ya kutunza mazingira, akisema kupanda miti ili kulinda uhai ni lazima na kupendekeza kazi ianzie ngazi za chini. Wanafunzi wafundishwe aina za miti ya asili na maeneo ya kuipanda, kisha waambiwe faida na hasara zake.

"Mimi nilisoma Shule ya Msingi Mengo Kibosho mkoani Kilimanjaro, miaka ya 1950 tulikuwa tunafundishwa aina za miti ya kupanda ili kuvuta maji ardhini na jamii za miti zinazoyahifadhi.



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mbeya, Gervas Nyaisonga ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC). **PICHA: MAKTABA**

Tuliiona na hata leo ninaifahamu. Kuna mikuyu na mifumo (mivumo) hii inapandwa kwenye vyanzo vya maji. Hilo halijabadilika," anasema.

Anasema waliijua miti na mahali pa kuipanda na faida zake na hasara zake iwapo ingetoweka. Aidha, walipanda misesewe ambayo ni dawa na miringaringa yenye majani mapana yanayoongeza mbolea ardhini na pia ni migumu inayofaa kwa ujenzi.

Anaongeza kuwa ili kuwe na programu yenye tija kampeni za kulinda miti zianze na malezi kwa kuwaonyesha wanafunzi shuleni na watoto nyumbani aina za miti, kuwapeleka mtoni, maeneo oevu (yenye maji) ili waone hasara, faida na kuelewa wanachotakiwa kukufanya.

"Leo tukisema tupande miti ni ipi? Ipandwe wapi? Miche iko wapi? Tusiseme tupande miti tuongeze uelewa na kuwa na ufasaha wa kila tunachotaka kifanyike kwa kuonyesha kivitendo." Anaongeza Askofu Amani.

"Tukisema miti ya asili tuwaonyesha wanafunzi na jamii inayopewa maagizo ili akili ielewe, moyo ukubali na tuwe wazalendo kwa sababu taifa ni letu wote. Kupenda nchi yako ni kuilinda pia."

Anataja aina za miti zenye manufaa kama 'gravilia na mikufi kupata mbao, 'cypress' kuezeka, 'pine' kupata mapambo kama miti ya Krimasi na pia inavuta maji. Aidha, anashauri jamii ipewe miche kwani watu wakiagizwa kupanda miti watapanda hata isiyo na tija, au inayoharibu mazingira mfano jamii za mikaratusi zinazodaiwa kukausha maji.

**KUWA MIFANO**

Askofu Amani anashauri wanafunzi wafundishwe sheria za mazingira, faida za kuzishika na kuziheshimu na viongozi wafanye kazi kwa kuonyesha mifano.

"Nilipokuwa Askofu wa Jimbo la Moshi mwaka 2008 nilisimamia kutunza mazingira kwa kuhakikisha kila anayepata Komunio ya Kwanza na Kipaimara anapanda mti, ustawi na uonekane," anasema.

Anaeleza kuwa watoto hao katika parokia za jimbo lake walipanda miti na alifanya hivyo ila kuwa na mkakati wenye tija na ulio endelevu.

Anasema hata Arusha anakofanyakazi sasa, upandaji miti unaendelea na ilipandwa kila parokia wakati wa kuzindua miaka 50 ya Umoja wa Wanawake Wakatoliki (WAWATA).

## WANENAVYO MALENGA

### MWANADAMU NAMUACHA

Mwanadamu namuacha, nachake hichokichaa,
Hivinasafishakucha, tumboni ninayo njaa,
Nasubiria kukicha, nifanye yanayofaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Usinirushie vocha, nisije zuabalaa,
Mjadala ninakacha, nisije nikachakaa,
Sumu alikwishaacha, iwe ze kunivagaa,
Mwanadamuhatihati, mwamini Mungupekee.

Kirusi UKIMWI kocha, madhara yake balaa,
Na hicho kila kukicha, kivingine chatambaa,
Ukitege kwenye bucha, chenyewe kinasambaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Namuona wangu pacha, kutoka najiandaa,
Zipu waziameacha, watu wanamshangaa,
Badala ya kumficha, picha ndiyo zasambaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Macho ninayafikicha, nione anapokaa,
Nyumba yake nipakacha, imejengwa kwa mkaa,
Mbona kuunguza picha, bila mafuta ya taa?
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Kiburi change naficha, nisijezua balaa,
Ninakwenda Kiraracha, kwenye baridi kukaa,
Hasira zitapoacha, nitazidi kushangaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Mipango kila kukicha, wewe uweze kupaa,
Hata madawa pekecha, pazuri uwezekaa,
Mungu nawangu uticha, wala sitalala njaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Utukufualiacha, akaja kwetu kukaa,
Kweli yake hakuficha, hata walipokataa,
Na kuonya hakuacha, watu waache tamaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Kukung'ong'a hataacha, hata kama wamfaa,
Mema kwako ataficha, ubaki unashangaa,
Aweza kutoakucha, ubaki unatambaa,
Mwanadamu hatihati, mwaminiMungupekee.

Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)
lwagha@gmail.com 0767223602

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### VITA NA IENDELEE

Kufa kweli kufaana, na vita iendelee,
Wengine wanauana, acha wao wapotee,
Wengine ndio wavuna, silaha wazipokee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Matamshi yapingana, hebu acha yatokee,
Wengineo wanaona, vita na iendelee,
Wengine wabishisana, wanataka ipotee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

DR Congo twaona, acha watu wachochee,
Watu wazidipigana, na maisha yapotee,
Huku wengine kuvuna, madini kuendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Amani wengi waona, itafanya walegee,
Sababu vita wanona, wabakiwa chekelee,
Silaha wauziana, pesa wajiongezee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Hata magonjwa twaona, yaache yaendelee,
Kama wote watapona, hizi kazi zipotee?
Dawa tunauziana, lazima ziendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Muuza ndizi twaona, ata kazi sipotee,
Nunua zote hapana, ni bora zimuozee,
Mzidi kuuziana, maisha yaendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Mpenyo akiuona, mlipuko utokee,
Itabaki kukutana, na kazi iendelee,
Wazidi kuvurugana, na kazi zisipotee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Endelea kupigana, hasara na zitokee,
Huku nyie mwauana, wengine wachekelee,
Faida wanaziona, wabakiwa zipokee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Ulaya wanapigana, shida kwetu zitokee,
Bei zavitu twaona, wengine wachekelee,
Wanavuna wanavuna, faida iendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## 'Changamkieni fursa mjikwamue kiuchumi'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAJASIRIAMALI wa Mkoa wa Dodoma wametakiwa kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi zilizoko ili kujikwamua kiuchumi.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, kwenye kongamano la kibiashara lililoandaliwa na wajasiriamali jijini hapo lenye lengo la kubaini fursa mbalimbali na mbinu za kibiashara.

Alisema Dodoma inakua kwa kasi kubwa na anatamani kuona wajasiriamali wakikimbilia fursa hizo ili kujiimarisha kiuchumi.

"Nipo tayari kuwashika mkono na kuwasaidia kufikia malengo yenu, nitaandaa utaratibu mzuri wa kushirikisha taasisi za fedha tukutane kwa pamoja tujadiliane namna nzuri ya uwezeshaji wa kimtaji," alisema.

"Rais Samia Suluhu Hassan anaendelea kutekeleza miradi mingi sana Dodoma ambayo inakuja na fursa kubwa za kiuchumi, hivyo ni jukumu lenu ninyi jumuiya ya wafanyabiashara kuzitambua na kuzichangamkia."

Naye Naibu Waziri wa Kilimo ambaye ni Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisisitiza wajasiriamali wenye sifa ya kukopesheka kupitia mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Jiji la Dodoma, watumie fursa hiyo ili kukuza mitaji yao na kuzifikia fursa nyingi za biashara kwa urahisi.

**"Nipo tayari kuwashika mkono na kuwasaidia kufikia malengo yenu, nitaandaa utaratibu mzuri wa kushirikisha taasisi za fedha tukutane kwa pamoja tujadiliane namna nzuri ya uwezeshaji wa kimtaji," alisema.**

# Serikali yatoa maagizo ASA uongezaji mbegu bora alizeti

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

SERIKALI imeiagiza Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA) kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za alizeti ili kukabiliana na upungufu wa mafuta ya kula uliokо nchini.

Akizungumza na Nipashe, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliitaka ASA kuhakikisha inazalisha angalau tani 5,000 za mbegu bora za alizeti mwaka huu na kufikia tani 10,000, mwakani.

Bashe alisema Wizara ya Kilimo, inatekeleza mpango maalumu wa kuondoa tatizo la upungufu wa mafuta ya kula nchini.

"Mkakati huu utafanikiwa kupitia kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za alizeti kwa wakulima, jitihada na mipango tunayoitekeleza kwa sasa inalenga kutuwezesha kufikia angalau kiwango za kuweza kuzalisha tani 15,000 za mbegu bora za alizeti ifikapo mwaka 2025," alisema.

Alisisitiza katika mwaka wa fedha wa 2022/23, serikali imejitahidi kuongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 200 hadi 900 ili kuchochea ufanisi wa sekta hiyo sambamba na uzalishaji wa mbegu bora za alizeti.

Pamoja na jitihada hizo, Waziri Bashe alisema wizara inatekeleza mkakati wa kupanua mashamba ya serikali ya uzalishaji wa mbegu ili kuhakikisha wakulima nchini wanatumia mbegu bora zitakazoongeza tija na mavuno.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alisema wamejipanga kuhakikisha wanafikia malengo waliyopewa na serikali katika uzalishaji wa mbegu bora za alizeti, pamoja na za mazao mengine.

"Wakala unamiliki jumla ya mashamba 13 ya kuzalishia mbegu yenye jumla ya hekari 16,588," alisema.

Alisema tatizo la mabadiliko ya tabianchi zimesababisha ASA kushindwa kutumia mashamba yake yote kwa ufanisi.

"Kwa mfano, kwa mwaka huu tumelazimika kuzalisha kwenye hekari 3,776.2 ambazo zinataratia kuzalisha kiasi cha tani 4,965.51 za mbegu," alieleza.

Dk. Kashenge alisema wakala umefanikiwa kuzalisha tani 2,088 za mbegu bora za alizeti zenye thamani ya Sh. bilioni 5.84 na kuzisambaza kwa wakulima katika mikoa 21.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Singida, Manyara, Dodoma, Kilimanjaro, Morogoro, Simiyu, Mara, Rukwa, Songwe, Iringa, Ruvuma, Tabora, Njombe, Mtwara, Lindi, Mbeya, Coastal, Kigoma, Katavi, Tanga na Shinyanga.

"Mahitaji ya nchi ya mbegu za alizeti kwa mwaka kwa sasa ni takribani tani za ujazo 5,252 wakati upatikanaji wa mbegu hizo kwa sasa ni tani 400 tu," alisema.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima (katikati), akiwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainabu Chaula (kushoto), pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Anna Henga (kulia), wakionyesha vitabu vyenye kupinga ukatili wa kijinsia walipokutana katika ofisi za wizara hiyo Mtumba jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Madiwani watakiwa kusimamia vyema sensa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, White Zuberi, amewataka madiwani kusimamia ipasavyo Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Zuberi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akihitimisha kikao maalumu cha wajumbe wa kamati za sensa ngazi ya kata kilichofanyika wilayani humo.

Alisema wanapaswa kutekeleza wajibu wao na kutojali lawama zitakazotokana na majukumu yao kwa mujibu wa mwongozo wa Sensa ya Watu na Makazi 2022.

"Naomba mhakikishe mambo yote yanaenda vizuri wakati wa zoezi hilo, sitegemei mgawanyiko fanyeni kazi kwa bidii na weledi," alisema Zuberi.

"Naomba muwe waadilifu, kwenye kazi hii kwa sababu kuna ambao hawataitwa lazima watakuwa wakifuatilia endapo kutakuwa na dosari ili waanze kukosoa."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Dk. Omary Nkullo, ambaye ndiye Katibu wa Kamati ya Sensa ya wilaya hiyo alisisitiza Waratibu Elimu Kata ambao kwa mujibu wa mwongozo ndiyo wenyeviti wa jopo la usaili katika ngazi hiyo, kuwa waaminifu ili haki itendeke.

"Inabidi tutafute utaratibu mzuri ili haki itendeke, tutaangalia utaratibu mzuri wa kuyafikisha maswali," alibainisha Dk. Nkullo.

Mmoja wa wajumbe, Mwalimu Safari Ndahani, alisema wameridhishwa na utaratibu uliowekwa na mwongozo wa sensa kitaifa ingawa tatizo lililojitokeza ni idadi kubwa ya waombaji ikilinganishwa na nafasi zilizotengwa.

"Tunasema utaratibu huu ni mzuri changamoto ni watu wengi walioomba, namna ya ufanyikaji usaili maana yake kwamba watu wengi walikuwa wanatamani wapate hizi ajira za muda, lakini sasa ajira zitakuwa chache," alisema.

Kwa mujibu wa mwongozo wa sensa ya watu na makazi 2022, madiwani ndio wenyeviti wa kamati za sensa ngazi ya kata na wamepewa jukumu la kuteua wajumbe wa jopo la usaili linaloshughulikia usaili wa makarani wa sensa na wasimamizi wa maudhui.





# Barabara Mbeya-Njombe yafunguliwa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI imeingilia kati na kufungua barabara inayounganisha mikoa ya Mbeya na Njombe kupitia Wilaya za Rungwe na Makete kwa lengo la kuwarahisishia usafiri wananchi wa maeneo hayo.

Uamuzi huo umekuja baada ya miaka minne kupita tangu wananchi wa Kata ya Luteba wilayani Rungwe waanze kulima barabara hiyo kwa kutumia jembe la mkono.

Wananchi wa Kata ya Luteba waliamua kulima barabara hiyo ili waitumie kufupisha umbali wa kwenda katika Hospitali ya Ikonda iliyopo wilayani Makete.

Endapo barabara hiyo itakamilika itawapunguzia wananchi hao umbali wa zaidi ya kilometa 104 wanazosafiri kwa sasa hadi kubaki kilometa tisa pekee.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Matari Masige, alisema kazi ya kufungua barabara hiyo imeshaanza na ipo katika hatua nzuri.

Alisema barabara hiyo ina urefu wa kilometa 9.5 na mpaka sasa zaidi ya kilometa 7.2 zimeshalimwa na mkandarasi anaendelea na kazi kumalizia kilometa mbili zilizobaki.

"Kwa sasa tunafanya kazi ya kufungua barabara hii yenye urefu wa kilometa tisa na nusu ambayo haikuwapo kabisa, kazi hii ikikamilika tunaanza awamu ya pili ya kuiimarisha kwa kujenga madaraja na makaravati na baada ya hapo ndipo itaanza kupitika kwa magari," alisema Mhandisi Masige.

Alisema kuwa barabara hiyo inajengwa kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. milioni 905 kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa wilaya ya Rungwe na Makete kusafiri kirahisi kwenda kwenye maeneo hayo.

"Kwa sasa wananchi wa Rungwe ili wafike Makete wanalazimika kuzunguka kupitia Kiwira, Isyonje, Igoma, Kikondo penye umbali wa kilometa 104 ndipo wafike mahali hapa, lakini barabara hii ikikamilika watasafiri umbali wa kilometa tisa pekee na hivyo watapunguza umbali na gharama pia," alisema Mhandisi Masige.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Atupele Mwakibete alitembelea barabara hiyo na kusema kuwa ni Sera ya Serikali kuunganisha mikoa yote nchini kwa barabara, hivyo ujenzi wa barabara hiyo ni mwendelezo wa sera hiyo.

Atupele ambaye ni Mbunge wa Busokelo alisema kuwa barabara hiyo ni mkombozi kwa wananchi wa jimbo lake, wilaya ya Rungwe na mikoa ya Mbeya na Njombe kwa vile pia itainua uchumi wa maeneo hayo.

"Barabara hii ni muhimu sana kuanzia kwenye huduma za kijamii, lakini hata kiuchumi pia, kwa sababu itasaidia kusafirisha bidhaa kama vile viazi, ndizi, ambazo zinapatikana kwa wingi katika wilaya hizi," alisema Mwakibete.

Alisema kuwa pia barabara hiyo itasaidia kukuza utalii kwenye Hifadhi ya Taifa ya Kitulo kwa kuwa itawezesha watalii wanaofika kutembelea hifadhi hiyo kupitia kirahisi kwenda kupumzika kwenye fukwe za Matema na Ngonga zinazopatikana katika mwambao wa Ziwa Nyasa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Swebe, alisema kuwa barabara hiyo ni muhimu hasa kwa wananchi wa Wilaya ya Makete ambao watapata fursa ya kufanya biashara na wenzao wa Rungwe.

"Wilaya ya Rungwe inalima ndizi kwa wingi, ukiangalia Makete wana uhitaji wa ndizi hivyo barabara hii pia itakuza biashara baina ya wilaya hizi mbili," alisema Swebe.

Alisema kuwa mbali na faida za kiuchumi na kijamii zitakazopatikana kutokana na kufunguka kwa barabara hiyo, pia itasaidia serikali ya wilaya hiyo kuwahudumia baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo ambao ili kuwafikia ilikuwa ni lazima kwanza upitie mikoa ya jirani.

"Tunayo kata yetu moja huku tulikuwa hatuwezi kuifikia mpaka tuzunguke kupitia mikoa mingine (hakuitaja) lakini kwa kufunguka kwa barabara hii sasa tutawafikia kirahisi na kuwahudumia," alisema Swebe.



Wananchi wa vijiji vya Mwaoga na Bwawani Kata ya Makongolosi mkoani Mbeya wakimsikiliza Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, katika mkutano wa hadhara uliofanyika juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wasaidizi wa sheria waombwa kusaidia wananchi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya imewaomba wadau zikiwamo taasisi za msaada wa kisheria kwenda kusaidia wananchi katika vijiji vyote vya halmashauri hiyo kupata sheria ndogo ambazo zitawawezesha kupunguza au kumaliza migogoro ya ardhi na ukatili wa kijinsia.

Ombi hilo lilitolewa juzi na viongozi wa Idara za Sheria na Maendeleo ya Jamii mbele ya wadau wanaotekeleza mradi wa Mwanamke Imara, unaolenga kuwapatia wananchi msaada wa kisheria na kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

Mradi wa Mwanamke Imara unatekelezwa nchini kwa ufadhiri wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) na wilayani Rungwa linaendelea katika kata tatu Kiwira, Kisondela na Masoko ambako wananchi wanapewa msaada wa kisheria.

Akizungumza mbele ya wadau hao, Ofisa Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Pongezi Sanga, alisema katika wilaya hiyo kuna migogoro mingi ya kijamii ambayo inahitaji uwapo wa sheria ndogo ili kukabiliana nayo.

"Katika wilaya yetu kuna migogoro mingi, lakini inayoongozwa kwa kuripotiwa ni ile ya ardhi na ukatili wa kijinsia, hivyo tunahitaji wananchi vijijini wasaidiwe kuandaa sheria ndogo ambazo zitawawezesha wao wenyewe kukabiliana na migogoro hiyo na ikibidi kuimaliza kabisa," alisema Sanga.

Alisema katika maeneo ambayo mradi huo unatekelezwa migogoro hiyo imepungua kwa kiwango kikubwa kutokana na wananchi kuwezeshwa kupata sharia ndogo zinazowaongoza wao wenyewe kwenye maeneo yao.

Kwa upande wake, Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Richard Pondo, alisema idadi kubwa ya vijiji wilayani Rungwe haina sheria ndogo hali ambayo inasababisha kuwapo kwa migogoro mingi inayoripotiwa kwenye vyombo vya dola ili itafutiwe ufumbuzi.

Alisema mchakato wa kuandaa sheria ndogo vijijini unahitaji gharama kubwa na kutokana na ufinyu wa bajeti, halmashauri haiwezi kuwawezesha wananchi wa vijiji vyote kupata sheria ndogo kwa wakati.

"Sisi kama halmashauri tunashindwa kuwasaidia wananchi wa vijiji vyote kupata sheria ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti, ingawa tumeanza katika vijiji vichache, lakini hatuwezi kuwafikia wote kwa wakati, hivyo ikiwezekana tunaomba wadau watusaidie katika hili," alisema Pondo.

Alisema kuwa vijiji vingi vina sheria chache ambazo zimepitwa na wakati, hivyo mchakato huo ni muhimu ukafanyika ili kuwasaidia wananchi kupata sheria mpya na kuboresha zile za zamani.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Rungwe, Omary Mungi, aliwataka wadau wanaofika wilayani Rungwe kwa lengo la kuelimisha au kutekeleza miradi mbalimbali kwa wananchi kuwatumia watu maarufu na wale wenye ushawishi mkubwa ili waweze kufanikiwa.

Aliwataja watu hao wenye ushawishi kwenye jamii ya wananchi wa Rungwe kuwa ni viongozi wa dini, wazee wa mila maarufu machifu na viongozi wa vijiji.

## Waiomba serikali kijiji kiunganishwe na makao makuu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Ikombe kilichoko Kata ya Matema, wilayani Kyela, wameiomba serikali iwajengee barabara ya kuunganisha kijiji hicho na makao makuu ya kata ili waondokane na usafiri wa kutumia mitumbwi ambayo inahatarisha maisha yao.

Wananchi hao wanadai kuwa wanashindwa kupata huduma muhimu ambazo zinapatikana Matema na hata kuvuka kwenda kupata huduma Kyela Mjini na maeneo mengine ya Mkoa wa Mbeya kwa sababu ya kukosa barabara.

Mmoja wa wananchi hao, Julius Angumbwike alisema walijaribu kuchimba barabara kwa kutumia jembe la mkono, lakini walikwama kutokana na jiografia ya eneo hilo kuwa na milima na mawe makubwa ambayo yaliwaletea shida.

Alisema barabara hiyo waliichimba pembezoni mwa Ziwa Nyasa na serikali iliwaahidi kuikamilisha barabara hiyo, lakini mpaka sasa haijatekeleza.

"Sisi huku biashara yetu kubwa ni vyungu na samaki, lakini wateja wetu wapo Kyela na Mbeya, sasa huwa tunalazimika kusafirisha kwa kutumia mitumbwi kwa sababu magari hayawezi kufika hapa," alisema Angumbwike.

Alisema hata uchumi wao unashindwa kukua kwa sababu ya kukosekana kwa usafiri wa uhakika na kuiomba serikali iwasaidie ili kukifungua kijiji hicho.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Jumbe, alisema alifanya ziara katika kijiji hicho akiwa ameambatana na maofisa wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kwa ajili ya kuangalia namna ya kujenga barabara hiyo.

Alisema tatizo la barabara hiyo ina milima yenye miamba mingi ambayo inatakiwa kupasuliwa kwa kulipuliwa na baruti pamoja na kuboresha madaraja na kuna mkandarasi alitakiwa aijenge barabara hiyo, lakini alitelekeza.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa wananchi wa kijiji hicho kwa sababu wananchi wa eneo hilo wanapata huduma muhimu katika maeneo ambayo wanalazimika kupita kwenye maji.

Pia, zingine za Kyela mjini zipo kwenye mipango ya serikali kujengwa na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati harakati za ujenzi zikiendelea.



**HABARI ZANZIBAR**

## Makarani sensa wakumbushwa kutumia lugha nzuri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid amewataka wakufunzi wa makarani na wasimamizi wa zoezi la sensa na makazi kuwa na lugha nzuri kwa wananchi ili kupata taarifa sahihi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa wasimamizi hao yaliyofanyika katika ukumbi wa Dk. Shein Tunguu nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema lugha nzuri ni jambo muhimu katika kupata taarifa sahihi kwa sababu bila ya lugha nzuri wananchi watashindwa kutoa ushirikiano.

Aliwataka wasimamizi hao kuwa waadilifu na kutunza siri ili kufanikisha zoezi hilo na kupata maendeleo.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema atakayebainika kuharibu kazi alizopewa katika zoezi hilo la sensa atafukuzwa kazi na kuchukuliwa hatua zingine za kisheria ikiwamo kushtakiwa.

Alisema serikali imetumia gharama kubwa katika kufanikisha zoezi hilo na hatasita kumchukulia hatua atakayeharibu.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema kuwa wanahitaji wasimamizi na makarani wa sensa wenye uwezo ili kufanikisha zoezi hilo.

Alisema ili ifanikiwe taarifa za watu zinahitajika kwa maendeleo ya uchumi wa nchi.

Kwa upande wake Kamisaa wa Sensa Zanzibar, Balozi Muhammed Hassan Hamza, alisema kuwa maandalizi ya sensa yameshakamilika na mwaka huu itakuwa ya aina yake kutokana na vifaa vitakavyotumika kuwa vya kidijitali.

Aidha, aliwataka wakufunzi hao kuwa wazalendo wa nchi hayo kwa sababu wanategemewa katika kutoa elimu ya nadharia na vitendo kwa makarani na wasimamizi wa sensa.

Zoezi la sensa ya watu na makazi linatarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

# Rais Mwinyi awaondoa hofu wajasiriamali mikopo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali haina tatizo na kikundi cha wajasiriamali kuongezewa kiwango zaidi cha mkopo, baada ya kumaliza malipo ya mkopo wa awali.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana katika Viwanja vya Shule ya Kiembe Samaki wakati alipoonana na kuzungumza na vikundi vya wajasiriamali mbalimbali waliopata mikopo kupitia fedha za Uviko -19, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake katika Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Alisema serikali haina tatizo na vikundi vya wajasiriamali vinavyokopesheka vinapohitaji kuongezewa kiwango zaidi cha mkopo baada ya kukamilisha malipo ya awali.

Alizitaka taasisi zinazosimamia utoaji wa mikopo hiyo kuendelea kutoa taaluma kwa wajasiriamali ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanakopeshwa.

Dk. Mwinyi aliwashukuru wajasiriamali wote walioanza kulipa mikopo yao, kukipongeza kikundi cha ujasiriamali cha usafi kutoka eneo la Michungwani kwa kufanikiwa kupata mkopo wa gari la kuzolea taka, ikiwa ni mafanikio makubwa kwao, kwa kuwa walianza kazi hizo kwa kutumia tolori.

Katika hafla hiyo Dk. Mwinyi alikabidhi gari la kuzolea taka kwa kikundi hicho.

Katika hatua nyingine Dk. Mwinyi aliweka jiwe la msingi la shule ya kimataifa ya 'ZAN COASTAL ACADEMY' iliyoko Nyamanzi ambayo inafuata mitaala ya Cambridge na kumpongeza mwekezaji wa shule hiyo kwa kuona umuhimu wa elimu, eneo ambalo lina manufaa makubwa kwa taifa.

Alisema taifa lolote lenye watoto walioelimika ni wazi kuwa litapiga hatua kubwa za maendeleo, akaahidi serikali kuendelea kushirikiana na sekta binafsi, kwa kutambua peke yake haiwezi kufanya kila jambo.

Alisema serikali itashirikiana na wawekezaji wa eneo hilo na kuchukua hatua ya kuzitafutia ufumbuzi changamoto ziliopo, ikiwamo ya miundombinu ya barabara na kwamba tayari kuna mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Fumba hadi Kisauni.

"Tunatambua umuhimu wa kuweka miundombinu katika maeneo hayo," alisema.

Alirudia kauli yake ya kuwataka wananchi waishio vijiji jirani na maeneo ya uwekezaji kuacha uvamizi kwa shughuli za ujenzi na kubainisha kuwa ni muhimu kwa uchumi wa taifa.

Aidha, Rais Mwinyi alitembelea mradi wa uhuishaji na uimarishaji wa majisafi katika eneo la Dimani na kuitaka Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa mujibu wa kikataba ilivyo.

Pia, aliwataka wananchi kuondokana na utamaduni wa kujenga pembezoni mwa barabara, kwa kuwa hatua hiyo huitatiza serikali inapotaka kuendeleza miradi mbalimbali, ikiwamo ya majisafi na salama.

Alisema kuna nyakati serikali hulazimika kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kulipa fidia ya majengo na vipando vya wananchi vilivyoko pembezoni mwa barabara zaidi ya gharama za mradi husika, hatua aliyosema wakati mwingine serikali hulazimika kuacha kutekeleza miradi hiyo.

Dk. Mwinyi alitembelea majengo ya shule iliyofanyiwa matengenezo makubwa katika eneo la Bweleo ambayo kabla ilikuwa inamilikiwa na mwekezaji kutoka nchini Korea na hatimaye kununuliwa na Serikali na akaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufikiria matumizi mazuri ya majengo ya shule hiyo.

Pia, alitembelea eneo la uwekezaji linalomilikiwa na wawekezaji wazalendo la AFRICAB liliopo eneo la Fumba linaloshughulika na uwekezaji wa hoteli pamoja na nyumba za kukodisha.



Baadhi ya washiriki wa mdahalo wa usalama wa waandishi wa habari na uhusiano wa Jeshi la Polisi wakimsikiliza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja, ACP Daniel Shillah (hayupo pichani), akifungua mdahalo huo uliofanyika Mjini Zanzibar, ambao umeandaliwa na Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kamanda awapa somo waandishi wa habari kujilinda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja ACP, Daniel Shillah, amewataka waandishi wa habari kufahamu hawapaswi kukaa katika kundi la waandamanaji zinapotokea vurugu badala yake wakae kundi la vyombo vya ulinzi na usalama.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mdahalo wa usalama wa waandishi wa habari na uhusiano na Jeshi la Polisi, ulioandaliwa na Umoja wa klabu za waandishi wa habari Tanzania (UTPC), Kijangwani mjini Unguja.

Alisema kuwa Jeshi la Polisi linapotuliza ghasia za vurugu hutumia nguvu za dola na kama waandishi wa habari watakaa katika kundi la waandamanaji watashindwa kuwafahamu na chochote kinaweza kuwapata.

Alisema kuwa katika hali kama hiyo waandishi wa habari huwa na sehemu yao maalumu ambayo hutakiwa kukaa ili kutekeleza majukumu yao ambayo hupaswa kukua katika kundi la vyombo vya ulinzi na usalama.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi na vyombo vya habari ni fani mbili tofauti na yenye maadili yasiyofanana ingawa baadhi ya muda hufanya kazi pamoja, ili kujenga jamii ya yenye kuzingatia utawala bora na haki za binadamu.

Alisema ingawa kuwa vyombo vya habari hutumiwa na vyombo vya usalama katika kuitoa hofu jamii, kupata usahihi wa taarifa iliyozagaa au uzushi ulioleta hofu katika jamii.

Alisema, miongoni mwa haki za binadamu ni kupata uhuru wa kupata habari, waandishi wa habari wanapaswa kushirikiana na wananchi kuhusu mambo mbalimbali ya kuleta maendeleo na kutatua changamoto za kijamii.

Kamanda huyo alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika jamii kuonesha mafanikio yaliyopatikana nchini.

Alisema wananchi wa kawaida hawawezi kupata nafasi ya kwenda kila mahala, kupitia waandishi wa habari wanaweza kujua maendeleo mbalimbali yanayoendelea.

Hata hivyo, alisema Serikali ya Zanzibar, inafanya mambo mengi ambayo yanapaswa kutambulika katika jamii, ikiwamo miradi ya maendeleo ya nchi katika maeneo tofauti ya Zanzibar, waandishi wa habari ni nyenzo muhimu kuimarisha uhusiano wa utendaji wa kazi.

Naye Katibu Mkuu wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) Mwinyimvua Abdi Nzukwi, alisema mdahalo huo umekusudia kujenga uhusiano mzuri kati ya makundi hayo na kujadili changamoto zinazojitokeza wanapokutana kufanya kazi pamoja.

"Kwa ujumla wake jukwaa hili litahusisha makamanda wa Polisi Tanzania nzima, Idara ya Mawasiliano ya Jeshi la Polisi, na waandishi wa habari," alisema.

Aidha, alisema lengo la mdahalo huo ni kuona watendaji wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi wapate uelewa namna ya vyombo vya habari vinavyofanya kazi na maadili yao, na pia waandishi wapate uelewa namna jeshi hilo na vyombo vya ulinzi vinavyofanya kazi.

Akiwasilidha mada katika kikao hicho, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Ramadhan Himid Haji, alisema uhusiano mzuri unahitajika kwa pande mbili hizo ili kuondoa ugumu hasa wa kutofanya kazi kwa kuaminiana.

Alisema Jeshi la Polisi ni chanzo kikubwa cha habari hasa kwa matukio yanayohusu uhalifu, akiitaka jamii na waandishi wa habari kushirikiana katika kukabiliana na uhalifu.

Aliwataka maofisa habari wa Jeshi la Polisi wawe na mtandao wa mawasiliano na waandishi wa habari pale tukio muhimu linapotokea bila ya kubagua vyombo vya habari.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa wa D'SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi na 1349/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MAIMUNA HAJI SASYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAJI ABDI SASYA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni yan usimamizi wa mirathi mahamaka za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 mwezi 07 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
**Zingatia.**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
**Imetolewa leo tarehe 15 mwezi 07 mwaka 2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**WILFRED NYAMWIJA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba P1688/0101 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BAHARI BEACH SECONDARY SCHOOL mwaka 2008** . kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**POLISI CONTROL NAMBA: 9910833590287**

## KUPOTEA KWA CHETI.



**JACQUELINE JONES SALEMA** anatangaza kupotea kwa cha kidato cha nne chenye index namba **S0227-0019** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **SPRING VALLEY SEKONDARI** mwaka **2017** iliyoko Mkoa Iringa kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi na taarifa ya **Polisi SO/RB/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI YA KIAPO CHA UPOTEVU

Mimi **MWAMSHIHIRI ABDULRAHMANI JUMA,** umri miaka 43, Dini Muislam, Kabila Mngindo, Mkazi wa Sinza, Mkoa wa Dar es salaam. Nikiwa na akili zangu timamu bila kushawishiwa na mtu yeyote Yule naapa na kuthibitisha kuwa :-
Mimi **MWAMSHIHIRI ABDULRAHMANI JUMA,** nathibitisha kuwa nimepotelewa na **HATI** halisi ya Nyumba **Plot Na. 780 block 'A'** iliyopo sinza wilaya ya Ubungo-Dar es salaam, katika mazingira ya kutatanisha HATI hiyo ilitolewa kwa majina ya marehemu **ABDUL JUMA ABDALLAHAMANI.**
Hivyo kwa kiapo hiki ninaomba mamlaka/taasisi husika inisaidie kupata **HATI** nyingine.
Nathibitisha kuwa yote niliyotamka ni kweli tupu, endapo lolote itathibitika kuwa ni uongo hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Sahihi ya mtoa kiapo

Kwa kuwa mtoa kiapo ni mtu mzima na mwenye akili timamu nakubali kiapo hiki.
**Kiapo hiki kimetolewa mbele yangu leo tarehe 05 mwezi 07 Mwaka 2022**

JINA
S.L.P
CHEO
SAHIHI
TAREHE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ADVENTINA KOKUTOA NKUBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK II** yenye **USAJILI NAMBA: T337 AAB, CHASSIS NAMBA: SX800016194, ENGINE NAMBA: 450759512.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI NAMBA: DAR/URA/RB/282954/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATAMUS ANANGISYE FUNGO,** Anatangaza kupotelewa na Kadi yake ya Gari aina ya **TOYOTA OPA** Yenye no za usajili **T 890 CMU CHASSIS NO ZCT100036568 ENGINE NO 1ZZ1056263** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo Chochote Cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/229270/2022**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA, KANDA YA BUKOBA**
**MAOMBI YA GHARAMA NA. 40/2022**
**YANAYOTOKANA NA KESI YA MAHAKAMA KUU SHAURI LA MADAI NA 1A/2002**
**ATHANAS SIMON ..............................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**KABANGA NICKEL CO. LTD ................MJIBU MAOMBI**
**WITO/ KUITWA SHAURINI.**

**Kwa KABANGA NICKEL CO. LTD Popote Ulipo**

Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la maombi ya madai ya gharama tajwa juu imepangwa kusikilizwa tarehe15 mwezi Agosti mwaka 2022 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mh. Jaji NGIGWANA wa Mahakama Kuu, Kanda ya Bukoba. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutohudhuria wewe wenyewe au mwakilishi wako, shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 14 mwezi Julai mwaka 2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
BUKOBA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANK JULIUS MTITU** Nyasubi mjini Kahama,anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 500 DTM** aina ya **M/RVR.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi. **KAH/RB/ 486/ 2022.**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA.**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.................OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE CHRISANT KAMUGISHA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION OF ESTATE**

**BY MAGRETH KIIZA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25th day of July 2022.

Dated at Bukoba this 08th day of July 2022.

REGISTRAR

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **EVEREST FREIGHT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX REVO** yenye namba za usajili **T.390 DFQ.** Yenye Engine namba **1GD4035899** na Chassis namba **MROBA3GD200102245.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi:**TAN/RB/283755/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **JUMA RAMADHANI HAMISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HUONIAO** yenye namba za usajili **MC 607 CBN.** Yenye Engine namba **157FMIJXA80178.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi:**TAN/RB/248910/2022.**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Watu tisa wauawa kwa risasi SA

**GAUTENG,** Afrika Kusini

POLISI nchini Afrika Kusini wanawatafuta washukiwa waliowaua watu tisa kwa kuwapiga risasi katika matukio mawili tofauti usiku wa kuamikia Jumapili ya wikendi iliyopita.

Taarifa ya polisi iliyotolewa jana ilisema watu wanne walivamiwa katika mkoa wa Gauteng na watu wenye silaha ambapo waliwamiminia risasi na kuwaua.

Katika tukio lingine tofauti mwili wa mwanaume mmoja ulipatikana katika jiji la Johannesburg ukiwa na majiraha ya risasi.

Taarifa hiyo inasema polisi wanaendelea na uchunguzi katika mkoa wa Cape Magharibi kubaini waliohusika na vifo vya watu watatu wa familia moja, huku mmoja akiwa si wa familia hiyo, katika mji wa Khayelitsha.

"Hawafahamau sababu ya mauaji hayo japo uchunguzi unaendelea," ilisema.

Afrika Kusini kwa majumaa kadhaa sasa imekuwa ikishuhudia mauaji yanayotekelezwa na watu wasiojulikana dhidi ya raia, watu 19 wakiuawa kwa risasi katika kipindi cha majumaa kadhaa yaliopita. **RFI**

## Ghana yathibitisha visa virusi hatari vya Marburg

**ASHANT,** Ghana

SERIKALI nchini Ghana imethibitisha visa viwili vya kwanza vya virusi hatari vya Marburg, ugonjwa unaoambukizana sana katika familia moja na virusi vinavyosababisha ebola.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) virusi hivyo viliua zaidi ya watu 200 nchini Angola mwaka 2005, mlipuko mbaya zaidi kuwahi kurekodiwa kulingana na Shirika la Afya Duniani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na BBC, wagonjwa wawili walifariki wiki iliyopita hospitalini katika eneo la kusini mwa Ashanti. Maofisa wa afya katika taifa hilo la Afrika Magharibi wanasema watu 98 sasa wako chini ya karantini.

Aidha, taarifa zinaeleza kuwa mpaka sasa bado hakuna matibabu kwa Marburg, huku madaktari wakishauri kunywa maji mengi na kutibu dalili maalum kutasaidia kukabili maradhi hayo.

Pia wataalamu wa afya walisema virusi hupitishwa kwa watu kutoka kwa popo wanaokula matunda na huenea kati ya wanadamu kupitia upitishaji wa maji ya mwili.

"Ni ugonjwa mbaya, ambao mara nyingi husababisha kifo na dalili kama vile maumivu ya kichwa, homa, maumivu ya misuli, kutapika damu na kutokwa na damu," walisema.

Maofisa hao wanaonya watu kujiepusha na mapango na kupika vizuri bidhaa zote za nyama kabla ya kuzila. **BBC**

# Hali ya dharura yatangazwa Sri Lanka

**COLOMBO,** Sir Lanka

KAIMU Rais wa Sri Lanka, Ranil Wickremesinghe, ametangaza hali nyingine ya dharura katika taifa hilo linalokumbwa na mzozo wa kiuchumi huku hatua hiyo ikitajwa kama njia moja ya kurejesha utulivu wakati bunge linapotarajiwa kumchagua rais mpya wiki hii.

**Wickremesinghe aliyeapishwa kuhudumu kama kaimu Rais, aliahidi kufuata sheria na kurudisha hali ya kawaida baada ya maandamano ya miezi kadhaa.**

Wickremesinghe alitangaza hali hiyo jana, akieleza kuwa hatua hiyo pia imechukuliwa kwa ajili ya usalama wa raia pamoja na kuwezesha usambazaji wa bidhaa muhimu kwa jamii.

Pia viongozi wanaokumbwa na utata nchini humo wamekuwa wakitangaza hali ya dharura kwenye taifa hilo tangu mwezi Aprili, wakati ambapo maandamano makubwa dhidi ya serikali yalipoanza kushuhudiwa huku malalamiko yakitolewa kutokana na kudorora kwa yali ya uchumi pamoja na upungufu wa bidhaa muhimu kama dawa na mafuta.

Askofu Jeewantha Peiris, mmoja wa viongozi wanaopanga mandamano nchini humo, alieleza kuwa hali ya dharura iliyotangazwa na kaimu Rais ni njia moja ya kutia uwoga waandamanaji kudai haki.

Aidha, hali ya dharura ilitangazwa nchini humo baada ya Rais wa nchi hiyo Gotabaya Rajapaksa aliyeondolewa madarakani kutoroka nchi yake kutokana na maandamano yaliyokuwa yakipinga utawala wake.

Taarifa zinasema Rajapaksa alitorokea nchini Maldives na kuelekea Singapore baada ya maelefu ya raia waliokuwa wanapinga utawala wake jijini Colombo kuvamia makazi na ofisi zake.

Wickremesinghe aliyeapishwa kuhudumu kama kaimu Rais, aliahidi kufuata sheria na kurudisha hali ya kawaida baada ya maandamano ya miezi kadhaa ya kulalamikia hali mbaya ya uchumi na ugumu wa maisha. **RFI**



Ranil Wickremesinghe akiapishwa kuwa Kaimu Rais wa Sri Lanka. **PICHA: AP**

# Maofisa 60 wafukuzwa kazi Ukraine

**KIEV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymir Zelenskiy, amewafuta kazi mkuu wa huduma za ujasusi na mwendesha mashtaka mkuu wa serikali akieleza kuwa watu 60 wanaotumikia taasisi zilizoongozwa na maofisa hao wanafanya kazi dhidi ya Ukraine katika maeneo yanayoshikiliwa na Russia.

Zelenskiy aliyasema hayo jana na kuongeza kuwa kesi 651 za jinai zimefunguliwa kuhusu madhambi ya uhaini wa kiwango cha juu zikiwahusisha wafanyakazi katika ofisi ya mwendesha mashtaka, vitengo vya kuchunguza kesi na taasisi nyingine za kisheria.

Pia alisema matukio hayo yanaibua maswali magumu juu ya maofisa hao waliofukuzwa, huku akisisitiza kuwa yote yatapata majibu sahihi.

Wakati huo huo jeshi la Russia lilitangaza kuwa limeziharibu silaha ambazo nchi za magharibi zimeipatia Ukraine, ukiwamo mfumo wa makombora wa Himars uliotolewa na Marekani, na hakuna upande huru uliothibitisha ukweli wa madai hayo ya Russia. **DW**

## Rais Samia amtumia salamu za rambirambi Ramaphosa

**DODOMA,** Tanzania

RAIS wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amemtumia salamu za rambirambi Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa kutokana na kifo cha aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Afrika Nation Congress (ANC), Yasmin Duarte, aliyefariki juzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Chama Cha Mapinduzi (CCM), Duarte enzi za uhai wake alikuwa ni kiongozi imara aliyesimamia misingi ya utu kwa ajili ya jamii yenye usawa bila kujali rangi, jinsia, wala utaifa ndani ya Afrika Kusini na duniani kwa ujumla.

Rais Samia alisema wako pamoja na Waafrika Kusini na duniani kwa ujumla ambao mbali na kuguswa na maisha ya kikazi ya Jessie, lakini walishirikiana naye katika kutekeleza wajibu wa kupigania na kulinda uhuru wa Mwafrika.

"Nimepokea taarifa za msiba kwa masikitiko makubwa salamu za rambirambi katika wakati huu mgumu ziwafikie familia yake, ndugu, jamaa na marafiki na wote waliioguswa na msiba huu," alisema.

Aliongeza kuwa kitendo cha Jessie kuwa msaidizi maalumu wa Hayati Nelson Mandela, mjumbe wa halmashauri kuu ya ANC na naibu katibu mkuu wa chama hicho tangu 2012 kinadhihirisha uwezo wa kiuongozi, uimara na umuhimu wake kwa ANC.

# MAJALIWA MGENI RASMI NBC MARATHON DODOMA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye mbio za NBC Dodoma Marathon zinazotarajiwa kufanyika Julai 31, mwaka huu.

**Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mjini Dodoma kuhusu hali ya maandalizi ya mbio za Marathon, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka alisema kuwa jiji hilo lina uwezo wa kutosha kuwapokea na kuwakarimu zaidi ya wageni 7,000 watakaofika mjini hapo kushiriki mbio hizo.**

"Nataka nimhakikishie kila mtu kuwa Dodoma iko tayari kuwapokea wakimbiaji wote na kukidhi matarajio yao. Tuna malazi, chakula na miundombinu ya kutosha kuhudumia wageni wote, wasiwe na wasiwasi wowote," alisema.

Mtaka pia alitangaza kuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa amekubali mwaliko wa kuwa mgeni rasmi wa mbio hizo zinazolenga kukusanya fedha za kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake nchini.

Mtaka pia aliwataka wananchi wa Dodoma kuzipokea mbio hizo kama dirisha la kiuchumi na kujiandaa kuendana na ongezeko la mahitaji ya kijamii.

"NBC Dodoma Marathon italeta karibu watu 7,000 mjini watahitaji chakula, malazi, mavazi, usafiri, na aina nyinginezo za burudani. Shime tuitumie fursa hii kujipanga vilivyo. Dodoma ina mengi ya kutoa; tuchangamkie fursa hiyo," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi alisema benki hiyo inafuraha kuandaa tena mbio zake jijini Dodoma baada ya mafanikio awali.

"Dhamira yetu ni kusaidia kuchangisha zaidi ya shilingi milioni 200 na kuzipeleka katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake nchini. Saratani ya Shingo ya Kizazi, ndiyo inayoongoza kwa kusababisha vifo vyingi zaidi vinavyohusiana na saratani kwa wanawake nchini Tanzania," alisema.

"Jambo la kutia moyo ni kwamba saratani hii inaweza kuzuilika na kutibiwa iwapo itagundulika mapema. Ni jukumu letu kwa pamoja kuunga mkono serikali yetu katika kuongeza uelewa," alisema.

Sabi pia alisema kuwa katika miaka miwili iliyopita, mbio za NBC Dodoma Marathon zimekuwa na mafanikio makubwa.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kulia), akipokea jezi ya NBC Dodoma International Marathon kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, ikiwa ni maandalizi ya kushiriki mbio za NBC Dodoma Marathon zitakazofanyika Jumapili, Julai 31 mwaka huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Dau dogo lamwondoa Malale Polisi

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale amesema dau dogo ni sababu kubwa ya yeye kushindwa kuendelea kukinoa kikosi kwa msimu ujao wa 2022/23 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Malale anahusishwa kukinoa kikosi cha timu ya Mbeya City kwa msimu mpya baada ya kocha wao, Mganda Mathias Lule kwenda kuwa msaidizi wa timu ya Singida Big Stars.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema baada ya kumaliza mkataba wake na Polisi Tanzania ameamua kuachana nao baada ya kupata ofa nzuri mmoja ya timu ambayo hakutaka kuweka wazi.

Alisema kuhusu kutajwa kwenda kuwa Kocha Kuu wa Mbeya City, hakuna ukweli na kuweka wazi kuwa ataenda kufundisha moja ya timu ya ligi ya Championships.

"Sio kweli bwana nakwenda timu ya daraja la kwanza (Championship), kwa sasa sikutajiji kwanza, ila kubwa nimemaliza mkataba na Polisi Tanzania na ofa nzuri imenifanya niende katika timu hiyo," alisema Malale.

Alisema amefanya maamuzi ya kwenda kufundisha Championships kwa sababu amepata ofa za timu tatu za Ligi Kuu na kwenda katika timu hiyo ambayo anafanya nao mazungumzo.

Taarifa kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Polisi Tanzania, Frank Lukwaro ilisema uongozo umefikia makubaliano ya pande zote ya kutoendelea na kocha Malale kwa msimu mpya wa 2022/23.

"Katika kipindi chake kocha Malale ameiwezesha timu yetu kumaliza katika nafasi mbalimbali za ligi na kutokana na mahitaji na tathmini iliyofanywa na uongozi wa timu imeamua kutafuta kocha mwingine," alisema Lukwaro.

## Nunda kusindikiza pambano la Kidunda

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Shafii Mohammed (Nunda) atazichapa na Joseph Masunga wakisindikiza pambano la 'Pay Back Night' kati ya Seleman Kidunda na Tshimanga Katompa kutoka DR Congo la kuwania mkanda wa WBF, linalotarajia kupigwa Julai 30, mwaka huu Songea mkoani Ruvuma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nunda alisema amejiandaa kufanya maajabu katika pambano hilo la utangulizi dhidi ya Masunga.

Alisema amejiandaa vizuri kwa lengo la kutaka kushinda pambano kwa kuwa hana hofu yoyote na mpinzani wake kutokana na maandalizi anayoendelea kuyafanya.

"Nimeajiandaa vizuri kuweza kushinda pambano langu, mpinzani wangu hawezi kumaliza raundi ya kwanza, maana nimefundisha kukanya watu hivyo akae akijua nakwenda kumkanya Songea," alisema Nunda.

Alisema itakuwa kazi nyepesi kwake kuwa anajua anachokifanya na kuwatoa hofu mashabiki wake kwamba, atamkalisha mapema mpinzani wake huyo.

Mapambano mengine ya utangulizi watakaopanda ulingoni kwenye pambano hilo ni Ismail Galiatano atazichapa dhidi ya Yamikani Mkandawile wa Malawi na George Bonabucha dhidi ya Yusuph Ally naye kutoka nchini Malawi.

## Geay apongezwa na serikali

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI imempongeza mwanariadha chipukizi, Gabriel Geay baada ya kushika nafasi ya saba kwenye mashindano ya mbio za Dunia za kilometa 42 yaliyofanyika Julai 15 mwaka huu, nchini Marekani.

Akizuñgumza jijini jana, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo, alisema mwanariadha huyo amefanya kazi kubwa kwenye mashindano hayo ambayo yameshirikisha nchi mbalimbali zenye wachezaji wazoefu.

"Sisi kama serikali tunampongeza amefanya kazi kubwa kuitangaza nchi yetu ni nafasi nzuri aliyoipata kwenye mashindano makubwa kama hayo, alisema Singo.

Mkurugenzi huyo alisema kwa upande wa serikali itaendelea kuwa bega kwa bega na mwanariadha huyo kuhakikisha wanamtimizia malengo yake ya kufika mbali zaidi.

Aliwataka wanariadha wengine waige mfano wake huo kwa kufanya mazoezi mara kwa mara ili wafikie uwezo wake.

"Ninaomba Watanzania waendelee kumuunga mkono Geay ninaamini siku zijazo ataifanyia makubwa nchi ya Tanzania kwenye mashindano mengine, alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KHAN AMTAJA KANE

OFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Khan amemtaja mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, kama "mshambulizi bora kabisa" na "ndoto ya siku zijazo" baada ya kukubali kumuuza Robert Lewandowski, 33, kwenda Barcelona. ***(Star)***

### KOUNDE ANUKIA BARCA

KLABU ya Barcelona imeelekeza nguvu zake kumleta mlinzi wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23, ambaye amekuwa akihusishwa na Chelsea, baada ya kufikia makubaliano ya kumnunua mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski. ***(Marca)***

### DE LIGT SAFI

BAYERN Munich wameweka ofa mpya ya pauni milioni 59.5 na pauni milioni 8.5 kama nyongeza kwa beki wa kati wa Juventus na Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22. ***(Goal)***

### TORUNARIGHA ATAKIWA

KLABU ya West Ham imetoa ofa ambayo haijawekwa wazi kwa ajili ya kumnunua beki wa Hertha Berlin, Jordan Torunarigha mwenye umri wa miaka 24 ***(Voetbal Nieuws)***

### DE JONG HATAKI

MCHEZAJI wa kimataifa wa Uholanzi, Frenkie de Jong anapinga kujiunga na Manchester United au klabu yoyote ya England, lakini kiungo huyo wa kati wa Barcelona mwenye umri wa miaka 25 anafikiria kuhamia kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich. ***(Sport)***

### DEPAY AWANIWA

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo tayari kulipa euro milioni 17 kwa mshambuliaji wa Barcelona, Memphis Depay, 28, lakini klabu hiyo ya Hispania inataka euro milioni 20, ingawa mchezaji huyo pia anasita kuondoka Nou Camp. ***(Sport)***

### DEPAY AJADILIWA

BODI ya Barcelona imefanya mazungumzo na Memphis Depay kubaini iwapo mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United ana nia ya kubaki au kuondoka. ***(Fabrizio Romano)***

### BROJA KUTUA WEST HAM

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Albania, Armando Broja atajiunga na West Ham kwa mkopo wa msimu mzima. Wagonga nyondo hao wa London walitaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 kwa mkataba wa kudumu, lakini The Blues walisita kumuuza mchezaji huyo ambaye alitumia msimu uliopita kwa mkopo Southampton. ***(Mail)***

### COLWILL KUONDOKA

MLINZI wa kati wa England, Levi Colwill, 19, atataka kuondoka Chelsea ikiwa klabu hiyo ya Stamford Bridge itasajili mabeki zaidi msimu huu. ***(Athletic)***

### THOMAS AGOMBEWA

KLABU za Portsmouth, Hibernian na Motherwell zinashindana kumsajili mchezaji huru, Terell Thomas, 26, baada ya beki huyo wa Saint Lucia kumaliza mkataba wake na Reading. ***(Hampshire Live)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DYBALA ATUA ROMA

**Ni baada ya Inter Milan kushindwa kupata saini yake, Mourinho ajitosa mazima...**

**ROME,** Italia

PAULO Dybala amekubali kujiunga na AS Roma msimu huu wa joto baada ya Inter Milan kushindwa kumsajili, kwa mujibu wa 90min.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 aliondoka Juventus mapema msimu huu wa joto baada ya kushindwa kukubaliana na masharti ya kuongezwa kwa mkataba na alihusishwa na timu kadhaa huku Inter ndio ikipewa nafasi kubwa zaidi.**

Hata hivyo, vyanzo sasa vimedokeza kwamba, Inter hawakuweza kutoa fedha zinazohitajika kukamilisha uhamisho wa Dybala, na kuiruhusu Roma kumnasa.

Inter wanadaiwa kujaribu kusitisha mkataba wa Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 33, ambaye ni miongoni mwa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi Serie A, lakini amefunga mabao 20 pekee katika mechi 108 alizoichezea Nerazzurri, lakini fowadi huyo wa zamani wa Manchester United alikataa ombi hilo.

Huku mishahara ya Sanchez ikiwa bado kwenye vitabu, Inter ilazimika kujiondoa kwenye mbio za kutafuta huduma ya Dybala, na Roma ya Jose Mourinho ikaingia kwenye mbio za kumwania.

Wapinzani wao Napoli pia walikuwa na hamu lakini ni Roma ambao watamsajili nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

Dybala alipendelea kusalia Serie A na hakuwa na nia ya kweli ya kuhamia England, ikimaanisha kuwa wawaniaji watarajiwa kama Manchester United waliondoa haraka jina lake kwenye orodha ya watu wanaotarajiwa kuwindwa msimu huu.

Kwa kujiunga na Roma, Dybala atakuwa na nafasi ya kufunga mabao 100 kwenye Ligi ya Italia.

Kwa sasa amefunga mabao 98 katika mechi 271 alizocheza wakati wote akiwa na Palermo na Juventus.

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,016,4

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 20-21 JULAI 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/07/22 | 18:00 | CA Fenix vs Mvo Wanderers | 2.39 | 3.02 | 3.12 |
| 02. 20/07/22 | 20:00 | Maccabi Haifa vs Olympiakos | 3.16 | 3.11 | 2.37 |
| 03. 20/07/22 | 20:00 | San Lorenzo vs Union Santa Fe | 2.44 | 3.18 | 3.07 |
| 04. 20/07/22 | 20:00 | Botev Plovdiv vs Apoel Nicosia | 2.88 | 3.23 | 2.42 |
| 05. 20/07/22 | 21:00 | Dynamo Kiev vs Fenerbahce | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 06. 20/07/22 | 21:15 | Maribor vs Sheriff Tiraspol | 2.79 | 3.09 | 2.64 |
| 07. 21/07/22 | 01:00 | Goias vs Fluminense | 3.24 | 3.19 | 2.26 |
| 08. 21/07/22 | 01:00 | CSA AL vs Cruzeiro | 3.18 | 2.93 | 2.41 |
| 09. 21/07/22 | 01:00 | Defensa Justicia vs Independiente | 2.30 | 3.23 | 3.28 |
| 10. 21/07/22 | 02:30 | Internacional vs Sao Paulo | 2.34 | 3.14 | 3.14 |
| 11. 21/07/22 | 03:30 | Lanus vs Velez Sarsfield | 2.82 | 3.12 | 2.67 |
| 12. 21/07/22 | 05:05 | Guadalajara Chivas vs Club Leon | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 13. 21/07/22 | 20:30 | Aris Limassol vs Neftchi Baku | 2.37 | 3.16 | 3.01 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO AKANUSHA KUREJEA SPORTING



**LISBON,** Ureno

CRISTIANO Ronaldo amepuuza uvumi kwamba, yuko mbioni kurejea katika klabu ya Sporting CP ya Ureno.

Ronaldo amewataka waajiri wa sasa Manchester United kusikiliza ofa kwa ajili yake msimu huu wa joto.

Sporting ni timu ya zamani ya Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, na ni miongoni mwa waliohusishwa na mshambuliaji huyo.


Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Ronaldo amekanusha madai hayo ya kurudi Sporting, akisema taarifa hizo ni uzushi.

Ronaldo amekosekana kwenye ziara ya United ya kujiandaa na msimu huu wa joto kutokana na 'sababu za kibinafsi' na akakosa nafasi ya kukutana na mchezaji mwenzake wa zamani Nani, ambaye alijitokeza kwenye ushindi wa Melbourne siku ya Ijumaa wakati kikosi cha Erik ten Hag kikinguruma kwa ushindi wa 4-1.

Baada ya mchezo huo, Nani alikiri kwamba, Ronaldo amekuwa akikwepa jitihada zake za kujaribu kujadili uwezekano wa uhamisho.

"Natumai (atasalia United)," alisema Nani.

"Ni mchezaji muhimu na mchezaji ambaye huwa analeta mabadiliko. Natumaini yuko katika hali nzuri ya kuisaidia klabu.



## Bayern yamtwaa De Ligt

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imefikia makubaliano na Juventus kwa ajili ya uhamisho wa beki wa kati wa Uholanzi, Matthijs de Ligt.

De Ligt alisajiliwa na wababe hao wa Italia mwaka 2019 baada ya kuiwezesha Ajax kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na wakati awali alikuwa nyuma ya Giorgio Chiellini na Leonardo Bonucci katika kikosi cha kwanza cha wababe hao wa Turin.

Kwa mujibu wa 90min, pande hizo mbili zimefikia makubaliano, ambapo Bayern watatoa euro milioni 80 na nyongeza ya euro milioni 10 - kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Mkataba wa miaka mitano ulikuwa tayari umekubaliwa na De Ligt, hivyo kilichobaki ni utibitisho wa kimatibabu tu.

De Ligt ataondoka Juventus akiwa amekaa kwa misimu mitatu na Bianconeri hao akicheza mechi 177 na kufunga mabao nane.

Alishinda taji la Serie A msimu wa 2019/20, lakini amekuwa sehemu ya kikosi cha Juve ambacho kilipitwa na AC Milan na Inter katika miaka ya hivi karibuni.

428,582/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/07/22 | 19:15 | Kortrijk vs OH Leuven | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 02. 23/07/22 | 21:30 | Hannover vs St. Pauli | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 03. 23/07/22 | 21:30 | Sarmiento vs Colon Santa Fe | 2.42 | 3.14 | 3.14 |
| 04. 23/07/22 | 22:30 | Vila Nova GO vs Vasco da Gama | 2.63 | 2.73 | 3.08 |
| 05. 24/07/22 | 00:30 | Nautico PE vs Londrina PR | 2.30 | 2.97 | 3.36 |
| 06. 24/07/22 | 02:30 | CRB AL vs Novorizontino SP | 2.48 | 2.93 | 3.08 |
| 07. 24/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs Nashville | 2.32 | 3.42 | 3.02 |
| 08. 24/07/22 | 02:30 | Orlando City vs Philadelphia Union | 2.37 | 3.43 | 2.93 |
| 09. 24/07/22 | 03:00 | Botafogo RJ vs Atletico Pr | 2.30 | 3.33 | 3.03 |
| 10. 24/07/22 | 03:00 | DC United vs Montreal Impact | 2.31 | 3.38 | 3.07 |
| 11. 24/07/22 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Los Angeles FC | 2.90 | 3.50 | 2.35 |
| 12. 24/07/22 | 05:00 | Vancouver Whitecaps vs Chicago Fire | 2.28 | 3.45 | 3.05 |
| 13. 24/07/22 | 12:00 | Tokyo Verdy vs Yokohama | 2.90 | 3.30 | 2.42 |
| 14. 24/07/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Magdeburg | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 15. 24/07/22 | 17:00 | Mechelen vs Royal Antwerp | 2.55 | 3.40 | 2.65 |
| 16. 24/07/22 | 22:00 | Westerlo vs Cercle Brugge | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 17. 24/07/22 | 22:00 | Juventude RS vs Ceara CE | 2.58 | 2.98 | 2.93 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 19 - JULAI 2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 1931 | Hebei Kungfu vs Shenyang City FC | 1.66 | 3.33 | 5.10 |
| 11:00 | 1947 | Shaanxi Changan vs Beijing BG | 1.45 | 4.30 | 5.67 |
| 12:30 | 2416 | Gold Coast Knights vs Logan Lightning | 1.23 | 6.07 | 8.03 |
| 13:00 | 1842 | SHB DA Nang vs Song Lam Nghe AN | 2.61 | 3.00 | 2.61 |
| 13:00 | 3472 | Dhaka Abahani vs Sheikh Jamal | 1.57 | 4.20 | 4.90 |
| 13:10 | 5296 | Manchester Utd vs Crystal Palace | 1.53 | 4.06 | 4.99 |
| 13:20 | 3656 | Japan vs Hong Kong | 1.01 | 12.72 | 34.25 |
| 14:00 | 2950 | M. Nam Dinh vs CLB Viettel | 3.52 | 3.33 | 1.94 |
| 14:00 | 3893 | Hai Phong vs SQC Binh Dinh | 2.21 | 3.09 | 3.09 |
| 14:30 | 1904 | Anhui Litian vs Suzhou Dongwu | 1.65 | 3.59 | 4.62 |
| 15:15 | 1368 | Sabah vs Terengganu | 2.65 | 3.25 | 2.55 |
| 16:00 | 3027 | Arsenal FC Reserve vs Racing Club Reserve | 2.75 | 3.15 | 2.39 |
| 16:00 | 3071 | Kedah vs Sarawak | 1.36 | 4.62 | 6.87 |
| 16:00 | 3333 | Independiente Reserve vs Defensa Y Justicia Reserve | 2.29 | 3.14 | 2.90 |
| 17:00 | 1089 | CA Tigre Reserve vs Patronato Reserve | 1.70 | 3.57 | 4.30 |
| 17:00 | 2073 | CA Central Cordoba SE Reserve vs CA Platense | 1.92 | 3.33 | 3.58 |
| 17:00 | 5926 | CA Union Santa Fe Reserve vs San Lorenzo de Almagro Res. | 2.50 | 3.24 | 2.55 |
| 19:00 | 1066 | Karabakh vs FC Zurich | 2.12 | 3.19 | 3.39 |
| 19:00 | 3291 | Skeid Fotball 2 vs Kjelsaas 2 | 1.44 | 4.82 | 5.11 |
| 19:00 | 4021 | Zalgiris vs Malmo | 4.70 | 3.55 | 1.71 |
| 19:00 | 5196 | Pyunik Yerevan vs Dudelange | 2.09 | 3.21 | 3.46 |
| 20:00 | 2148 | Norrby IF vs Jonkopings Sodra | 1.62 | 4.03 | 5.10 |
| 20:00 | 2347 | Orgryte IS vs Brommapojkarna | 2.90 | 3.56 | 2.30 |
| 20:45 | 3276 | Ludogorets Razgrad vs Shamrock Rovers | 1.35 | 4.51 | 8.42 |
| 20:45 | 3323 | Midtjylland vs AEK Larnaca | 1.38 | 4.41 | 7.62 |
| 21:00 | 1422 | KF Tirana vs Zrinjski Mostar | 2.45 | 3.07 | 2.97 |
| 21:00 | 1952 | Hibernians vs Levadia Tallinn | 3.23 | 3.33 | 2.18 |
| 21:00 | 3458 | Liverpool (URU) vs Albion FC | 1.52 | 3.93 | 5.30 |
| 21:00 | 5428 | Ferroviaria SP U20 vs Santos SP U20 | 3.09 | 3.14 | 2.18 |
| 21:00 | 5560 | XV De Novembro SP U20 vs Gremio Osasco Audax EC U20 | 1.93 | 3.34 | 3.54 |
| 21:45 | 1304 | Elgin City vs St Johnstone | 6.30 | 4.43 | 1.40 |
| 21:45 | 1697 | Queens Park vs Dundee FC | 3.28 | 3.38 | 2.00 |
| 21:45 | 2085 | Dumbarton vs Raith Rovers | 3.53 | 3.53 | 1.87 |
| 21:45 | 2407 | Annan Athletic vs Ayr United | 4.50 | 3.87 | 1.61 |
| 21:45 | 3681 | Stirling vs Aberdeen | 9.22 | 5.30 | 1.25 |
| 21:45 | 4042 | East Fife vs Buckie Thistle FC | 1.38 | 4.71 | 6.08 |
| 21:45 | 4147 | Montrose vs Stenhousemuir | 1.87 | 3.59 | 3.49 |
| 21:45 | 4322 | Inverness vs Albion Rovers | 1.20 | 5.68 | 10.76 |
| 21:45 | 4668 | Alloa Athletic vs Ross County | 4.90 | 4.21 | 1.52 |
| 21:45 | 4801 | Linfield Belfast vs Bodo Glimt | 5.59 | 3.99 | 1.54 |
| 21:45 | 4959 | La Fiorita vs KF Ballkani | 12.05 | 5.63 | 1.24 |
| 21:45 | 5227 | Airdrieonians vs St Mirren | 6.27 | 4.31 | 1.41 |
| 21:45 | 5516 | Partick Thisle vs Fraserburgh | 1.15 | 6.30 | 13.78 |
| 21:45 | 5826 | Cove Rangers vs Kelty Hearts FC | 1.73 | 3.68 | 4.02 |
| 21:45 | 5882 | Forfar Athletic vs Stranraer | 1.89 | 3.38 | 3.63 |
| 22:00 | 1730 | Dinamo Zagreb vs Shkupi Skopje | 1.10 | 7.60 | 25.02 |
| 22:15 | 4399 | KR Reykjavik vs Fram Reykjavik | 1.54 | 4.23 | 4.62 |
| 22:30 | 5623 | CA Platense vs Central Cordoba | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 22:30 | 5773 | Colon Santa Fe vs Aldosivi | 1.78 | 3.39 | 4.13 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KMC YASEMA HAISAJILI WACHEZAJI MITANDAONI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imesema haisajili wachezaji wake kwa kutafuta sifa mitandaoni, badala yeke inasajili kimya kimya bila makeke na itaanza kumtangaza mmoja mmoja zoezi hilo litakapokamilika.

**Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, amesema mpaka sasa wanaendelea vizuri na usajili, ingawa wao hawapigi kelele kama klabu zingine.**

"Wao wanasajili wanatangaza sijui saa saba mchana, saa sita usiku mara saa tisa, sisi hatusajili mitandaoni, tunasajili ofisini, kocha akisema tunamtaka huyu, tunamwita ofisini tunamsajili. Hao wanaofanya hivyo zote hizo mbwembwe tu, mwisho wa siku mchezaji ataonekana uwanjani tu," alisema Mwagala.

Mwagala amesema hakuna klabu yenye kutunza siri nchini kama KMC mpaka sasa hakuna mwandishi wala mchambuzi anayeweza kupata taarifa hata tetesi ya kwamba mpaka sasa wamemsajili mchezaji gani na watawaacha kina nani.

"Siyo kama hatusajili, tunasajili na wapo wachezaji tukaowaacha, lakini kwetu huwezi kusikia hata tetesi, huko kwingine Dodoma Jiji, Simba, Yanga, Azam wanapata kwa sababu wao usajili wao ni wa mbwembwe wengine wanachapisha kwenye mitandao ya kijamii, wengine wanafanya sherehe, kwa hiyo haijalishi, hata wakodishe ukumbi na kufanya tafrija kwa ajili ya kumtambulisha mchezaji ni sawa tu, ila sisi tumechagua staili hii. Tukimaliza, tutaanza kumtambulisha mmoja mmoja," alisema Mwagala.



Wachezaji wa Timu ya Cambiasso Sports wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Ujenzi wa viwanja utainua vipaji – Mwinyi*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameeleza kwamba ujenzi wa viwanja vya michezo vya kisasa hapa Zanzibar kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuinua vipaji kwa vijana.



Mwinyi (pichani) aliyasema hayo juzi baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa viwanja vya michezo unaojengwa na Kampuni ya F.L.A ya wawekezaji wazawa vilivyopo Kisakasaka, Shehia ya Kombeni Jimbo la Dimani, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mwinyi pia alitumia fursa hiyo kutoa pongezi kwa vijana walioanzisha mradi huo wa viwanja vya michezo na kueleza hayo ndio maono yake katika suala zima la viwanja vya michezo.

Alisema kuwa viwanja vinavyotakiwa kujengwa hivi sasa ni vyenye mfano kama huo ambavyo vina sifa ya kuweza kutumika usiku na mchana na vyenye mazingira mazuri.

Alisema kwamba yeye ni muumini wa michezo na kusisitiza azma ya Serikali ya kujenga viwanja kama hivyo vya kisasa ambavyo vitakuwa vikitumika wakati wote na kuhusisha michezo mbalimbali ukiwamo mchezo wa 'Go-karting'.

Aliongeza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwaunga mkono vijana hao ili waweze kuendesha vizuri mradi wao huo.

Aliwapongeza viongozi wa Mkoa na Wilaya kwa usimamizi mzuri wa kuhakikisha mradi huo unafanikiwa huku akiwaahidi kwamba wateja wengi watawapata mara tu watakapoanza shughuli zao za michezo katika viwanja vyao hivyo.

Naye msimamizi wa 'The Legend Sport Centre' Fahmi Moh'd Abdi alimweleza Rais Mwinyi jinsi hatua zilivyochukuliwa katika ujenzi wa viwanja hivyo wakati akimtembeza katika eneo hilo.

Michezo
Jumanne Julai 19, 2022
Nipashe




Ronaldo akanusha kurejea Sporting UKURASA 22



Nyota wa Simba, Clautos Chama (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Ismailia FC ambayo inashiriki Ligi Kuu ya Misri kwenye mchezo wa kirafiki baina ya timu hizo, juzi. **PICHA: SIMBA SC**

# KOCHA SIMBA SC ATOA MSIMAMO

**Na Saada Akida**

## Asema hajali matokeo kwenye mechi za kirafiki, anahitaji kujenga timu kwanza...

KOCHA Mkuu wa Simba, Zoran Manojkovic, amesema hajali sana suala la matokeo katika mechi yao ya kirafiki kwa sababu anahitaji kuona aina ya timu yake kwa ajili ya kuimarisha msimu mpya wa 2022/23.

**Simba juzi ilicheza mechi ya kwanza ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Ismailia FC, na kutoka sare ya 1-1 mchezo uliopigwa katika dimba la Ismailia, nchini Misri.**

Bao la Simba likifungwa na Augustine Okrah ikiwa ni bao lake la kwanza tangu alipojiunga na klabu hiyo kwa msimu huu wa mashindano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zoran alisema mechi wanazocheza kwa ajili ya kuona na kupata mwanga wa kikosi chake na ana imani baada ya mechi nne zijazo zitamsaidia kufanya vizuri zaidi.

Alisema hajalishi matokeo anayoyapata zaidi ya kuhitaji kuona timu yake inapata michezo ya kirafiki kwa kuona upungufu na uwiano wa wachezaji wake.

"Ni kweli tumecheza mechi ya kirafiki matokeo sio muhimu sana kwa sababu nahitaji kuona wachezaji wangu licha ya wachezaji kutokamilika wote, nina imani mechi zijazo zitatusaidia kufanya vizuri zaidi," alisema Zoran.

Katika hatua nyingine Ahmed Ally alisema klabu imefika makubaliano ya kumwongezea mkataba mpya wa miaka miwili kiungo mkabaji wao, Mzamiru Yassin.

Alisema kupitia ripoti ya mwalimu amerishishwa na kiwango cha kiungo huyo kupewa mkataba mpya kutumikia timu hiyo kwa msimu ujao.

"Mzamiru atakuwapo katika kikosi cha Simba, tunaendelea kukiimarisha kikosi ikiwamo kuongeza mikataba ya wachezaji ambao tunaamini bado ni msaada mkubwa kwetu," alisema Ahmed Ally.

# Okrah aahidi makubwa Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji mpya wa Simba, Augustine Okrah, amewaahidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutarajia makubwa kutoka kwake, baada ya kufunga bao lake la kwanza akiwa na kikosi hicho kwenye mechi ya kujipima nguvu dhidi ya Ismailia ya Misri juzi.

Okrah ambaye alifunga bao kwenye mechi ambayo timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, alisema mechi haikuwa mbaya sana, na walicheza huku wakiwa hawajafanya mazoezi kwa muda mrefu.

"Ni mechi ya maandalizi tu ya msimu, haikuwa mbaya, nawashukuru sana wachezaji wenzangu walionipa msaada mkubwa kwenye kufunga bao hilo langu la kwanza kwenye timu hii, ni furaha kwangu na mashabiki wa Simba, nataka kuongeza kiwango changu na kufanya zaidi ya hili kwa ajili yangu na mashabiki wa timu," alisema.

Kwenye mechi hiyo, Okrah alisema yalikuwa ni maelekezo ya kosa kumtaka asicheze sana pembeni, badala yake aningia ndani na kucheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, badala ya winga, ndipo alipofanikiwa kufunga bao hilo.

"Ulikuwa ni uamuzi wa kocha, alinipa maelekezo ya kuingia ndani, badala ya kucheza pembeni sana na ndiyo ilinisaidia kupata bao. Kuhusu kuendelea kufunga nitafanya hivyo zaidi, kwa sababu hiyo ndiyo kazi yangu," alisema Okrah, raia wa Ghana akihojiwa jijini Ismailia baada ya mechi hiyo kumalizika.

Mchezaji huyo alitangazwa kusajili na Simba hivi karibuni, moja ya usajili ambao ulizua gumzo si Tanzania tu, badi Afrika nzima.

Wakati huo huo, wachezaji watano wa Simba waliosalia nchini wamewasili na jana walitarajia kuanza mazoezi na wenzao.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema wachezaji, Moses Phiri, Enock Inonga, Peter Banda, Thadeo Lwanga na Nassor Kapama waliwasili wakitoka nchini baada ya kukwama kwa sababu mbalimbali tofauti.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >